# MIFANYIKO YA KIFONOLOJIA KATIKA KINYALA CHA KAKAMEGA

Na:

**SITETI wa NGERO**

Tasnifu hii imetolewa ili kutosheleza baadhi ya mahitaji ya shahada ya "Master of Arts" katika Chuo Kikuu cha Egerton.

EULIB
021 052

1996

**UNGAMO**

"Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijatolewa kwa mahitaji ya digrii katika chuo kikuu kingine chochote."

---

**SITETI wa NGERO**

Tasnifu hii imetolewa kutahiniwa kwa idhini yangu kama msimamizi wa kazi hii wa chuo kikuu.

---

**USTADH ROCHA MUZUNGU CHIMERAH**

## HATILINZI

Kuna hatilinzi. Hakuna sehemu ya tasnifu hii ambayo itatoleshwa, kuhifadhiwa katika mfumo wowote ule kwa minajili ya kutoleshwa, au kunakiliwa, katika umbo au njia yoyote ile, iwe ya kielektroniki, kiukarabati ama kurekodiwa bila idhini ya mwandishi na Chuo Kikuu cha Egerton.

# MUHTASARI

Tasnifu hii imejadili mifanyiko ya kifonolojia katika Kinyala cha Kakamega, hususan jinsi mifanyiko hiyo inavyodhihirika kwa kuiundia kanuni zinazoitawala. Kazi hii, mbali na kuziainisha sauti za Kinyala (K), inaibua muundo wa kifonolojia wa lahaja hii. Ni kutokana na uainishaji wa sauti na uibuaji wa muundo wa kifonolojia ndipo yeyote yule atakaye kujifunza au kufunza lahaja hii anaweza kufanya hivyo kwa utaratibu ufaao. Mifanyiko ya kifonolojia katika Kinyala cha Kakamega ndio lengo la tasnifu hii.

Sura ya kwanza ni utangulizi wa utafiti huu. Miongoni mwa mambo mengine, somo la utafiti limejadiliwa, madhumuni ya utafiti na pia sababu za kulichagua somo hili. Zaidi ya hayo, nadharia ambayo imetumiwa kama msingi wa utafiti huu imezungumziwa. Mwisho, njia za utafiti ambazo zilitumiwa kufanikisha utafiti huu zimejadiliwa.

Sura ya pili inajadili maandishi mbalimbali yanayohusiana na somo hili.

Sura ya tatu inajadili sauti za Kinyala cha Kakamega. Hii inatokana na dhana inayosisitizwa na Mario Pei (1965:11) kwamba ambapo fonolojia inaweza kufafanuliwa kama uchunguzi wa sauti za lugha vile zinavyobadilika na kugeuza umbo katika maendeleo ya lugha, fonetiki ndiyo sayansi, uchunguzi, uchanganuzi na utabakishaji wa sauti za lugha bila kurejelea maendeleo yake kihistoria; lakini kwa kurejelea utamkaji, uenezaji na upokeaji

wake. Yaani, fonolojia na fonetiki huchanganiana kiasi kwamba ni vigumu kuzungumzia fonolojia bila kurejelea fonetiki. Hivyo basi, katika sura hii, mfumo wa kifonetiki wa Kinyala cha Kakamega umejadiliwa na kuziainisha sauti zote za lahaja hii - konsonanti na vokali.

Sura ya nne imejadili mifanyiko ya kifonolojia katika Kinyala cha Kakamega. Sura hii imejaribu kuonyesha jinsi na pale ambapo mifanyiko hiyo hutokea na kuieleza kiisimu. Katika kufanya hivyo, iliundiwa kanuni mwafaka zinazoambatana nayo (mifanyiko).

Sura ya tano ni ya kuhitimisha. Sura hii imepitia kazi yote kwa jumla na kuonyesha kwamba Kinyala cha Kakamega hudhihirisha mifanyiko ya kifonolojia ya aina nane. Fauka ya hayo, matatizo yaliyoukumba utafiti huu yamejadiliwa na kutoa mapendekezo ya maswala ambayo yanastahili kufanyiwa utafiti zaidi.

## SHUKRANI

Ningependa kutanguliza shukrani zangu za dhati kwa msimamizi wangu katika kazi hii, Ustadh Rocha Muzungu Chimerah, ambaye, mbali na kutosita kulikubali hili jukumu, bila maongozi, maelekezo na ushauri wake mwema kuhusu mada hii, kazi hii haingefikia daraja hili la ufanisi. Ukarimu, uangavu na uwajibikaji wake ulinifaa sana, kiasi kwamba tulishauriana mahali popote pale tulipokutana.

Pili, ningependa kuwashukuru wafadhili wangu, Dkt. Kimani wa Njoroge, Dkt. Bernard Kitur, Bw. Njogu Waita na Kasisi Boaz Chombe (Mungu amrehemu), kwa kujitolea ima fa ima kunifadhili ili niweze kuingilia kazi ya shahada ya digrii ya pili. Wahadhiri wote wa Idara ya Lugha na Ismu - Chuo Kikuu cha Egerton - hawafai kusahauliwa. Mbali na usaidizi mwingine, walinitia shime na hamasa kwa kuchangia vilivyo, hasa, wakati wa kozi na kuandika pendekezo la utafiti wangu. Msaada wao ulinifungulia milango ya mbinu za kufanya utafiti wa kisomi. Miongoni mwa wahadhiri hawa, ningependa kuwataja na, inapowezekana, majina yao yaenezwe na kuangaza kama siraji kokote kule duniani kwenye wasomi kindakindaki. Ustadh Chacha Nyaigotti Chacha, Bw. Onyango Ogolla, Bi. Rosemary Imbosa Liguyani, Bw. F.O.B Aswani, Bw. Joshua Simiyu Njasi, Bw. George Mwaro, Bw. Gwachi Mayaka, Bw. Evans Mirieri na Bw. Furaha Tchai, ambao majadiliano yangu nao, kuhusu pendekezo la utafiti, yalikuwa ya manufaa si haba. Himizo la Ustadh Chris Lukorito Wanjala wa Idara ya Fasihi halitasahaulika milele.

Isitoshe, ningependa kutoa shukrani zangu kwa Chuo Kikuu cha Egerton kwa kugharimu masomo yangu ya digrii ya M.A kwa miaka miwili. Mkuu wa Chuo hiki, Ustadh J.C Kiptoon, na naibu wake anayesimamia Utafiti na Maenezi, Ustadh Chris Onyango, wanastahili heko kwa kuchukua hatua ya kuniruhusu nijiunge na jumuia ya wasomi, licha ya pingamizi kutoka pembeni pembeni. Bila msaada huo, kazi hii, labda, isingekuwa kama ilivyo sasa au haingekuweko asilani.

Ningependa shukrani nyingine ziwaendee Wanyala wa Kakamega wote ambao, kwa pamoja, walinisaidia sana kwa kunipa habari kuhusu historia ya Wanyala na kunichangia msamiati si haba. Bila usaidizi wao, utafiti wangu usingefanikiwa kama ulivyofanikiwa sasa maadam umri wangu ni makamo na singeweza kuelewa chochote kuhusu jamii hii hapo kabla. Ningependa kuwashukuru Mabwana Ngero wa Egesa, Francis Ngero, Moris Mayende, Siteti Leo, Mulindo Wenje, Barasa Kombo, marehemu Makhupe Mulindo, Geoffrey Ngero, Oyavira Leo, Siteti Oyavira, Alexander Wanjala, Mumia Mukhwana, Cheng'ole Ngero, Humphrey Egesa, Doreen Nanyama, Ben Sikenyi, Ernest Muchana, Joseph Wawire Sarifu "Kokoto" na Bi. Nawire Siukho, ambao walinisaidia katika uelewaji wa historia ya Wanyala (K) na lugha yao.

Pia, ningependa kuwashukuru Mabwana Manoah Mukhwana (EMC), Malick Maina Shanguya, Shadrack Okila Okwiri, Willis Otieno Opoto, Dkt. Malilo Barasa, Dkt. Francis N. Wegulo, Bi. Edith Oyiela, Bi. Ann Wanjiru Muchoki, Bi. Violet Odenda, Bi. Dorcas Waruguru, Bi. Rachael Wanjohi na Bi. Mildred "Emily" Otieno, kwa msaada wao.

Siwezi kuwasahau Mabw. Stephen Otuchi na James Mbugua, Mabibi Brigid Gitonga na Mary Namiti kwa msaada wao wa kuniachia nafasi ya kutumia vifaa katika EMC kwa utafiti wangu. Bila msaada wao, utafiti huu haungefanikiwa.

Vile vile ningependa kuwashukuru wanafunzi wenzangu katika kozi ya M.A kwa mijadala ya kiakademia tuliyokuwa nayo, ambayo ilituelekeza ipasavyo katika ulimwengu wa usomi wa utaalam. Sitasahau wakati mgumu wa kuamka kabla ya kupambazuka tuliovumilia nao kwenye safari ya Bewa la Laikipia. Hawa ni akina Mutuku Kavoi, Sheila Wandera na Jane Nguru. Ogoti Ongarora na Jascinta Ndambuki hawawezi kusahaulika ninapofikiria mijadala yetu.

Mwisho kabisa, ningependa shukrani zangu ziwaendee Mabibi Miriam Maina, Cynthia Mmene na Olga Aduma ambao, licha ya kwamba nilifanya kazi ya kupiga chapa mimi mwenyewe, wao pia walinisaidia hapa na pale. Bila msaada wao, wa kujitolea kufanya kazi ya ziada, kazi hii isingefanikiwa na kufikia kiwango hiki cha ufanisi.

Kwa wengine ambao, kwa bahati mbaya, sikuwataja majina, isiwe kwamba nina utovu wa shukrani. Kwa yeyote aliyehusika sana au chembe na kazi hii au nami kama binadamu, ninasema shukrani kwa jumla.

**AHSANTENI NA ALHAMDULILAHI**

## TABARUKU

Naitabarukia kazi hii kwa babangu, **NGERO wa EGESA,** na mamangu, **NAKHUMWA mukha NGERO**, ambao ingawa hawakupata fursa ya kuhudhuria angalau darasa la kwanza walinipa motisha na msukumo, kwanza, kwa kutoa chochote walichokuwa nacho kunielimisha na, pili, kwa kunitia shime masomoni, hadi kumaliza kazi hii. Kwa mwanangu mpenzi, **DOREEN NANYAMA NGERO**, na mke wangu, **EDITH OYIELA**, ambao waliniliwaza wakati wa ukiwa na uvunjifu. Mwanangu, **NAKHUNGU wa NGERO**, ambaye, kutokana na umri wake, hakuweza kufahamikiwa na hali ya babake ambaye alimwacha kiasi cha kutupwa, alivumilia na kubakia kuwa kimbilio langu na kihimili na kumbusho la umuhimu wa kujibidiisha, angalau arithi chochote.

# FAHARASA


Ukurasa

Mada ya Utafiti.............................. i
Ungamo....................................... ii
Hatilinzi.................................... iii
Muhtasari.................................... iv
Shukrani..................................... vi
Tabaruku..................................... ix
Faharasa..................................... x
Dibaji ya Michoro............................ xii
Dibaji ya Viambatanisho...................... xiii
Istilahi Zilizotafsiriwa..................... xiv

**SURA YA KWANZA: UTANGULIZI**

1.0 Utangulizi............................... 1
1.1 Somo la Utafiti.......................... 4
1.2 Madhumuni ya Utafiti..................... 4
1.3 Sababu za Kulichagua Somo Hili........... 5
1.4 Tahadhanio............................... 6
1.5 Maswali ya Utafiti....................... 6
1.6 Msingi wa Nadharia....................... 7
1.7 Upeo wa Utafiti.......................... 11
1.8 Njia za Utafiti.......................... 13
1.9 Maelezo ya Istilahi...................... 16

**SURA YA PILI: YALIYOANDIKWA KUHUSU SOMO HILI**

2.0 Utangulizi............................... 17
2.1 Yaliyoandikwa Kuhusu Somo Hili........... 17
2.2 Hitimisho................................ 29

**SURA YA TATU: SAUTI ZA KINYALA (K)**

3.0 Utangulizi.......................... 30
3.1 Konsonanti za Kinyala (K)............. 34
3.2 Vokali za Kinyala (K)................. 46
3.3 Mfuatano wa Sauti katika Kinyala (K).. 51
3.4 Hitimisho............................. 66

**SURA YA NNE: MIFANYIKO YA KIFONOLOJIA**

4.0 Utangulizi............................ 67
4.1 Wiano................................. 67
4.2 Mifanyiko ya Miundo ya Silabi......... 77
4.3 Kudhoofika na Kupata Nguvu............ 81
4.4 Usawazisho Changamano................. 88
4.5 Tabdili............................... 90
4.6 Usigano............................... 91
4.7 Haplolojia............................ 92
4.8 Sandhi................................ 93
4.9 Hitimisho............................. 94

**SURA YA TANO: MUHTASARI NA HITIMISHO**

5.0 Utangulizi............................ 95
5.1 Kazi kwa Jumla........................ 95
5.2 Mafanikio na Matatizo................. 97
5.3 Mapendekezo........................... 98
Marejeleo............................. 100
Viambatanisho......................... 108

## DIBAJI YA MICHORO

Mchoro 1: Ala za Sauti........................... 31

Mchoro 2: Chati ya Konsonanti za Kinyala (K).......... 43

Mchoro 3: Chati ya Vokali za Kinyala (K).............. 48

Mchoro 4: Mahali pa Kutamkia Vokali za Kinyala (K)... 48

## DIBAJI YA VIAMBATANISHO

Kiambatanisho 1: Alama Rasmi za Kifonolojia.......... 108

Kiambatanisho 2: Deta................................ 112

Kiambatanisho 3: Bajeti.............................. 119

Kiambatanisho 4: Ratiba ya Utafiti................... 122

# ISTILAHI ZILIZOTAFSIRIWA

| **Kiswahili** | **Kiingereza** |
|---|---|
| Fonolojia Zalishi Geuzaumbo | Transformational Generative Phonology |
| Fonolojia Zalishi Asilia | Natural Generative Phonology |
| Usilimisho | Assimilation |
| Muundo wa Silabi | Syllable Structure |
| Kupata Nguvu na Kudhoofika | Strengthening and Weakening |
| Usawazisho Changamano | Neutralisation |
| Usigano | Dissimilation |
| Tabdili | Metathesis |
| Haplolojia | Haplology |
| Sandhi | Sandhi |

# SURA YA KWANZA

## UTANGULIZI

### 1.0 UTANGULIZI

Kiluyia ni lugha ya Kibantu ambayo wazungumzaji wake, kihistoria, wanajulikana kama Wabantu wa Magharibi (Were, 1967). Wanyala, kwanza, walitamakani Busia na, hatimaye, kutengana baada ya matatizo ya kisiasa, kijamii na kiuchumi, ambapo kundi moja lilikumbwa na mabadiliko ya lugha kutokana na taathira kutoka makundi mengine ya Kiluyia waliyokurubiana nayo, katika hekaheka za uhamiaji kutoka Busia hadi makao yao sasa, Navakholo.

Wanyala (K) walitoka Busia katika sehemu ya pili ya karne ya kumi na tisa (Were 1967). Madai haya yanapewa uzito na ukweli kwamba, hadi sasa, kuna msitu huko Busia unaojulikana kama Olukaka lwa Maero. Maero ndiye aliyewaongoza Wanyala wa Kakamega katika harakati zao za uhamiaji. Baada ya kupitia nchi ya Wawanga, Wanyala walifika Emakokhwe, ambapo walitulia kabla ya kutawanyika katika pembe kadhaa za pale panapoitwa hivi sasa, Bunyala ya Kakamega.

Utengano uliozuka huko Busia, kwa hivyo, ulisababisha Wanyala, kwa jumla, kugawika katika makundi mawili: Abanyala ba Kisakati na Abanyala ba Mukhamba (Wanyala wa Mukhamba). Wanyala wa Kisakati, ambao pia wanajulikana kama Abanyala Baongo, waliitwa Wanyala wa Kisakati kuzingatia jina la mama. Hawa walibakia Busia na kuongea Kinyala Kiongo. Wanyala wa Mukhamba, ambao walihamia

Kakamega, waliitwa hivyo kuzingatia jina la baba. Hawa huongea Kinyala cha Mukhamba. Uainishi huu ni muhimu kwa sababu kuna makundi mawili yanayodai kuongea Kinyala.

Kutokana na maelezo hayo, tunaona kwamba licha ya kwamba kuna lahaja mbili tofauti za Kinyala, hii si ithibati tosha ya kuzua madai kwamba Kinyala ni lugha inayojisimamia. Madai imesemekana kuwa kwamba lahaja inapokua na kuvyaza lahaja nyingine inakuwa lugha. Walakini hiki si kigezo pekee cha lugha.

Wanyala wa Kakamega wanaweza kupigwa mafungu mawili muhimu, ambayo ni Abasiondo na Abayima. Abasiondo, ambalo ni kundi la mashujaa, pia wanaitwa Abanju ba Esimbo, yaani watu wa fimbo - silaha. Kundi hili hujumlisha makundi kama vile Abamuchuu, Abasaya, Abamisoho, Abauma, Abasiondo, Abatabani, Abalinda Bioki na Abaero. Abayima hujumlisha makundi kama vile Abatecho, Ababenge, Abasia, Abaengere, Abaucha, Abakwangwachi, Abasenya, Abasiroli, Abaafu, Abaumo, Abakangala, Abasonge, Abasamama, Abamwaya, Abayaya, Abakonga na Abairifuma. Abairifuma na Abasenya ni makundi yaliyotokana na Wamaasai, madai ambayo yanatiliwa uzito na usemi kwamba mahali ambapo Wanyala wa Kakamega walihamia yalikuwa makazi ya Wanandi na Wamaasai - Abaseve. Ingawa hivi leo neno Abaseve huhusisha Wakikuyu, ni muhimu itajwe kwamba Wanyala wa Kakamega walikuwa na ukurubiana finyu sana na Wakikuyu. Mbali na Wamaasai na Wanandi, ambao walisaidia nyakati za vita dhidi ya Wakabras, walihusiana, kwa kiasi, na Wang'oma (Sabaot au Bongomek). Kuna makundi mengine ambayo, licha ya kwamba hayakuwa ya Wanyala mwanzoni, hivi sasa wamekubaliwa kama Wanyala. Makundi

haya ni kama vile Abakekere na Abasamango, ambao waliishi miongoni mwa Wanyala na kuzua kundi lao; Abaalira, ambao, inasemekana kuwa ni Waganda au walitoka Uganda; na Abaolo, ambao yadaiwa ni Wajaluo kutoka Uholo, Siaya.

Ingawa Wanyala (K) wanaweza kugawanywa katika makundi madogomadogo, wote wanajichukulia kama jamii moja iliyounganishwa na mambo kadhaa. Kwanza, hawa ni watu walio na historia inayolandana. Pili, watu hawa wana mifumo sawa ya kijamii ikiwemo mila, utamaduni na itikadi. Tatu, mifumo yao ya kiuchumi inashabihiana ambapo wote ni wakulima na wafugaji. Nne, walikuwa na mfumo sawa wa kiutawala, kwanza, chini ya Maero, aliyewaongoza kutoka Busia na, pili, walikuwa chini ya Manyuru, chifu wao wa kwanza baada ya kutamakani Navakholo, ambaye aling'olewa madarakani baada ya kumuua mkewe. Baadaye, Ndombi Tavasi alichukua hatamu za uongozi na kuwatesa sana Wanyala, jambo ambalo liliwaletea umoja kama kundi la watu waliodhulumiwa. Tano, tangu zamani na hadi wa leo, watu wote hawa wanaongea lugha moja inayojulikana kama <u>Kinyala cha Mukhamba</u>.

Kinyala (K), kwa hivyo, ni lahaja ya lugha inayoongewa na kundi moja la watu wajulikanao kama Waluyia, chambilecho Angogo (1983). Kinyala kinachorejelewa hapa ni kile kinachoongewa na kundi la Wanyala waishio katika Mkoa wa Magharibi wa Kenya, Wilaya ya Kakamega, Taarafa ya Navakholo.

## 1.1 SOMO LA UTAFITI

Utafiti huu ulichunguza mifanyiko ya kifonolojia katika Kinyala cha Kakamega.

Nia ilikuwa kudhihirisha kuwa Kinyala, kama lugha nyingine ile, hupitia mifanyiko ya kifonolojia. Katika kufanya hivyo, muundo wa kifonolojia wa Kinyala (K) uliibuliwa na mifanyiko inayodhihirika katika lahaja hiyo.

Kwa jumla, mada hii ilielekeza kwenye uchunguzi wa mifanyiko ya kifonolojia katika Kinyala (K), hususan, jinsi mifanyiko hiyo inavyoweza kuelezwa katika misingi ya kiisimu, kwa kuiundia sheria au kanuni zifaazo.

## 1.2 MADHUMUNI YA UTAFITI

Katika kuchunguza mifanyiko ya kifonolojia katika Kinyala (K), utafiti ulilenga kueleza sauti zipatikanazo katika lahaja hii na mifanyiko itokeayo. Pia utafiti huu ulilenga kuonyesha jinsi mifanyiko hiyo hutokea kwa kuiundia kanuni ambazo hufuatwa kuifikia. Utafiti huu, kwa hivyo, ulitekeleza majukumu manne muhimu.

1. Kubainisha mifanyiko ya kifonolojia.

2. Kuieleza mifanyiko hiyo kiismu.

3. Kuiundia sheria za mazingira ambayo mifanyiko hiyo hutokea.
4. Kuibua muundo wa kifonolojia wa lahaja hiyo.

## 1.3 SABABU ZA KULICHAGUA SOMO HILI

Kama ilivyosemwa hapo awali, Kinyala (K) kimepitia mabadilliko mengi ambayo yamejikita katika mifanyiko ya kifonolojia.

Kuna uwezekano wa kukisia kwamba mpangilio wa kifonolojia hutukia kiasilia tu ila hutingwa na mwanda wa kifonolojia wa mzungumzaji. Hili ni jambo lifaalo kurejelewa kwa makini kwa sababu, katika hali fulani, sheria za kifonolojia hudhihirishwa katika mpangilio wa kifonolojia, ambacho ni kijelezi muhimu cha kuelezea vizuizi vipatikanavyo katika uzungumzaji na uelewaji wa asilia. Katika hali kama hii, imedaiwa kwamba uzingativu wa mabadiliko husaidia mwanafonolojia kuelewa mpangilio na muumano uliopo.

Utafiti huu unatarajiwa kuzua ilhamu ya utafiti na uvumbuzi wa kifonetiki na kifonolojia ambapo, awali, uchambuzi wa kifonetiki ulijikita sana katika uelezaji wa jinsi na mahali pa kutamkia sauti fulani. Hata hivyo, wanaismu kama vile Fry (1970), Laver (1972) na wengineo wamependekeza kuwa yafaa kuwe na uvumbuzi wa kimethodolojia, na kuongeza kuwa uchambuzi wa kifonolojia unatakiwa upanue mipaka yake na kuhusisha jinsi ya kupokea uzungumzi na jinsi unavyoratibiwa. Kwa hivyo, fonolojia itafungua milango ya fonetiki.

Suala la sifa bainifu ni muhimu sana katika utafiti huu. Kutokana na uchunguzi uliofanywa na baadhi ya wanaismu kama vile Lass (1984) na Anderson (1985), mzozo kuhusu mifumo ya sifa bainifu haujasuluhishwa. Kwa hivyo, utafiti huu huweza kusaidia katika kutathmini uwafaka au uwezekano wa nadharia yenye nguvu, kama

vile ilivyodokezwa na wanafonolojia asilia kama vile Hooper (1976) na Foley (1977).

Mbali na umuhimu wake kinadharia, utafiti huu unaweza kudhihirika katika utendakazi wake, kwani mambo yapatikanayo katika utafiti wa aina hii huweza kutumiwa kutatua matatizo maalum kuhusu sehemu maalum. Nyanda husika hapa ni kama vile: uundaji upya wa kifonolojia wa ndani kwa ndani katika taaluma ya filolojia (Anderson 1973); mbinu ya kuchunguzia makosa katika muktadha wa ufundishaji wa lugha (James 1980); na utambuzi mpya katika usasaishi wa lugha, chambilecho Eastman (1983).

Matokeo ya utafiti huu yatawafaa sana wanasarufi, walimu wa lugha na wapangaji wa lugha kufikia uamuzi ufaao.

## 1.4 TAHADHANIA

Kinyala (K), kama lugha nyingine yoyote, huwa na mifanyiko ya kifonolojia na, mifanyiko hiyo inaweza kuelezwa kiisimu.Kwa hivyo, tahadhania ni kuwa:

1. Mifanyiko ya kifonolojia katika Kinyala (K) ni ya kifonimiki.

2. Kanuni za kifonolojia zinaweza kutumika katika kuchunguza fonolojia ya Kinyala (K).

## 1.5 MASWALI YA UTAFITI

Kwa mujibu wa tahadhania, utafiti huu ulinuia kujibu maswali yafuatayo:

1. Je, lahaja ya Kinyala (K) hudhihirisha mifanyiko ya kifonolojia?

2. Je, mifanyiko ya kifonolojia, katika lahaja hii, ni ya kifonimiki?

3. Je, mifanyiko ya kifonolojia, katika lahaja hii, inaweza kusawiriwa na kuelezwa kiisimu?

4. Je, kanuni za kifonolojia zinaweza kutumiwa kueleza mifanyiko ya kifonolojia katika lahaja hii?

## 1.6 MSINGI WA NADHARIA

Utafiti huu ulifaidi, si haba, kutokana na Fonolojia Zalishi Asilia (Natural Generative Phonology - NGP).

Nadharia ya Fonolojia Zalishi Asilia iliendelezwa sana na Theo Vennemann na kufafanuliwa na Hooper (1976) na hurejelea mambo matatu muhimu:

i) Hali imara ya uasilia (a strong naturalness condition)
ii) Hakuna hali ya upangaji (a no-ordering condition)
iii) Hali halisi ya makisio ya kijumla (a true generalisation condition)

### 1.6.1 Hali Halisi ya Makisio ya Kijumla

Kipengele muhimu sana cha nadharia ya fonolojia zalishi asilia ni kile cha hali halisi ya makisio ya kijumla, ambayo inajulikana

kwa Kimombo kama <u>True Generalisation Condition</u> (TGC). Kipengele hiki, sana sana, huzingatia hali kwamba kuna uwezekano wa kuwa na kanuni zote zielezazo hali angavu za makisio ya kijumla ambayo ni ya kweli au halisi kwa maumbo yote yaonekayo/yadhihirikayo na, isitoshe, kwamba uhusiano kati ya maumbo yanayodhihirika wazi yaelezwe kwa njia iliyowazi iwezekanavyo.

Nadharia inayojumlisha hali hii huzingatia sana kule kuondoshwa au kupunguzwa, kwa kiasi kikubwa, udhahania uwezao kudhihirishwa na muongeaji mahsusi wa lugha husika.

Jambo jingine muhimu ni kwamba mbinu hii, ya kutilia vizuizi dhana ya uwezekano wa kuweko na sheria zinazoeleweka wazi, hujitokeza kila moja ikiwa na sifa zake. Sheria za kimsingi ni sheria za kifonolojia zinazohusisha [P-]; sheria za sandhi ambazo hurejelea mipaka ya maneno au mofimu; sheria za mofofonimiki [MP-] ambazo huhusisha michakato yote inayozingatia kanuni za kimofosintakiti kuzua vibadala vya kifonolojia; sheria zinazopitia [ ⟷ ] ambazo huonyesha uhusiano kati ya mofimu au vibadala vya kimofosintakitiki vinavyofanana k.m. divine/divinity huweza kuhusishwa na kanuni /ai/ ⟷ /i/ ingawa kila umbo linaweza kuorodheshwa kibinafsi katika leksia; uainishaji wa maandishi kimofolojia na sheria za uundaji maneno. Aina za sheria huzingatia uchunguzi stadi wa uelezaji rasmi wa sheria hizo.

Uangavu wa hali hii unaendelezwa katika utekelezaji wa sheria hii katika hali ya kutopanga.

### 1.6.2 Hakuna Hali ya Upangaji

Hali ya kutopanga hurejelea jinsi sheria hizi zinavyotumika. Nadharia ya Fonolojia Zalishi Asilia (FZA) hupendekeza kuwa sheria hutumika moja baada ya nyingine, pale ambapo hujitokeza zaidi ya moja mara moja, lakini si katika mpangilio funge. Kinachorejelewa hapa ni kwamba sheria huweza kutumika kwa umbo au muundo fulani (Structural Description rules - SD) - Sheria za Kimuundo (SK).

Katika Kinyala (K), sauti /p/ hutamkika kama /p / katika neno "para" (fikiri) na kutamkika kama /b/ katika neno "mbara" (ninafikiri) au katika "pukha" (chafuka) → "mbukha" (ninachafuka), "pima" (pima) → "mbima" (ninapima) n.k. Hali hii inaweza kuelezeka:

$$\begin{bmatrix} +\ \text{Kituo} \\ \\ -\ \text{Ghuna} \end{bmatrix} \longrightarrow \begin{bmatrix} +\ \text{Kituo} \\ \\ +\ \text{Ghuna} \end{bmatrix} /[+\ \text{Nasali}]____$$

Kwa hivyo, ni muhimu kwamba turuhusu muundo wenyewe uzue ruwaza zinazotumiwa bila kulazimisha mpango maalum.

### 1.6.3 Hali Imara ya Uasilia

Mbali na hali ya upangaji wa sheria, hali halisi ya makisio ya jumla ina vizuizi vinavyohusiana na jinsi ya uwasilishaji wa maumbo. Makisio ni kwamba hakuna sheria za kidhahania na, hivyo basi, hakuna haja ya kuwa na vipandesauti au sifa za kidhahania. Kutokana na jambo hili, fonolojia zalishi asilia imedokeza hali imara ya uasilia.

Hali imara ya uasilia huhitaji kwamba uhusiano kati ya maumbo na viwakilishi vyake lazima uwe wa moja kwa moja. Hakuna sifa ambazo yafaa zijitokeze katika uwasilishaji wa kileksia wa mofimu, isipokuwa zile zipatikanazo katika uwasilishaji wa kifonetiki. Kinachosemwa hapa ni kwamba maumbo yanayowasilishwa yafaa yazingatie sifa maalum za kifonetiki. Jambo hili laweza kuelezwa na vituo ambapo:

$$[- \text{Ghuna}] \longrightarrow [+ \text{Ghuna}] / [+ \text{Nasali}]___$$

Mifano hapa inapatikana katika maneno:

| | | | |
|---|---|---|---|
| [para] | "fikiri" | [mbara] | "ninafikiri" |
| [tola] | "okota" | [ndola] | "ninaokota" |
| [kana] | "tamba" | [ŋgana] | "ninatamba" |
| [tʃola] | "dondoa" | [ɲjola] | "ninadondoa" |

Tunaona wazi kwamba kuna sifa moja tu ambayo imefanyiwa marekebisho, ambapo tunapopata neno "para" (fikiri) tunaona likiwa "mbara" (ninafikiri). Haya ni mageuzi asilia ambayo yanatuelekeza kwenye fonolojia asilia.

### 1.6.4 Swala la Uhalisia

Anderson (1985) ameshughulikia sana hili swala la nadharia asilia na kutoa madai kwamba kuna mambo ya kijumla na asilia yanayohusiana na mifumo yote ya kifonolojia, na kwamba kuna uwezekano wa kutafuta maelezo ya hali ya michakato kwa kuzingatia uwezo wa kifonetiki wa mwanadamu. Uwezo huu unatokana na hali kwamba uzungumzi hupangwa na kuongozwa na bongo na viungo au ala zinazotumika katika utamkaji.

Nadharia ya Fonolojia Zalishi Asilia imekashifiwa na baadhi ya wataalam kwamba haijitoshelezi. Walakini, hakuna nadharia yoyote inayojitosheleza bila kuchangiwa hapa na pale. Tunabakia kukubaliana na pendekezo la Wolfram na Johnson (1982) kuwa, kwa kiwango fulani, nadharia hii inatutolea mwangaza kuhusu jinsi tunavyoweza kuelewa maelezo ya kifonetiki bila kupuuza mahitaji halisi ya uelezaji kwa uketo.

## 1.7 UPEO WA UTAFITI

Utafiti huu ulifanywa katika Taarafa ya Navakholo, Wilaya ya Kakamega. Ilipobidi, ulijishughulisha na Wanyala wa Busia, pale ambapo mifanyiko katika lahaja hizi inashabihiana.

Wakiongea juu ya sarufi ya lugha, Fromkin na Rodman (1988:17) wanasema:

> Sarufi hujumlisha kila kitu wanachojua wazungumzaji kuhusu lugha yao - mfumo wa sauti ambao unajulikana kama fonolojia; mfumo wa maana unaojulikana kama semantiki; kanuni za uundaji maneno unaojulikana kama mofolojia; na kanuni za uundaji sentensi unaojulikana kama sintaksia (tafsiri ni yetu).

Kutokana na maoni hayo, ni muhimu itajwe kuwa utafiti huu ulijikita katika fonolojia. Taaluma ya fonolojia inapozingatiwa, lugha hutazamwa kama muungano wa mambo mawili - vipandesauti na vile ambavyo si vipandesauti (Catford 1977a). Somo hili lilizingatia vipandesauti vinavyodhihirika katika kanuni asilia. Uchunguzi huu ulijikita katika mifanyiko ya kifonolojia na kanuni zifuatwazo katika kufikia mifanyiko hiyo.

Walakini, kuna uwezekano wa kuwa na vizuizi fulani katika utafiti huu. Kwanza, ni muhimu itajwe kuwa uchunguzi huu ulizingatia lahaja moja tu ya Kinyala badala ya zote mbili, ambazo, awali, zilichukuliwa kuwa za Kiluyia na kuhesabiwa kuwa miongoni mwa kumi na saba, ambazo Angogo (1983) ameziainisha katika makundi matatu:

KILUYIA

| KASKAZINI | | KATI | | KUSINI | |
|---|---|---|---|---|---|
| Kibukusu | Kisamia | Kiwanga | Kinyore | Kiidakho | Kimaragoli |
| | Kinyala(K) | Kimarama | Kitachoni | Kiisukha | |
| | Kinyala(B) | Kitsotso | | Kitiriki | |
| | Kikhayo | Kikisa | | | |
| | Kimarachi | Kikabras | | | |

Kwa sababu za upeo wa somo, ni vigumu kufanya uchunguzi wa kijumla unaohusiana na vipandesauti vya lugha. Kwa hivyo, ni mifanyiko ya kifonolojia tu ndiyo ilizingatiwa katika uchunguzi huu.

Ingawa Kinyala cha Busia kina uhusiano wa karibu sana na Kinyala cha Kakamega, swala hilo halikuwa la kimsingi katika utafiti huu. Jambo hili latokana na hali kwamba kuzama katika masuala ya isimu historia kati ya hizi lahaja mbili ni jambo la nje katika utafiti huu.

## 1.8 NJIA ZA UTAFITI

Utafiti huu ulijiegemeza kwenye mbinu za utafiti wa nyanjani wa hali halisi katika Taarafa ya Navakholo. Kwa mintarafu hii, ilitubidi kuishi Navakholo, miongoni mwa Wanyala (K) wakati wote wa utafiti na kuzuru pembe nyinginezo katika Wilaya ya Kakamega wanakopatikana waongeaji wa lahaja hii ili kupata ulinganisho ufaao wa mifanyiko ya kifonolojia. Hata hivyo, utafiti huu ulizingatia mbinu nne maalum za ukusanyaji deta zifaazo. Mbinu hizo ni:

### 1.8.1 Uundaji wa Chati ya Kifonetiki

Mbinu hii ilitumiwa katika kuzieleza sauti zote zipatikanazo katika lahaja hii. Mbinu hii ilitokana na ukweli kwamba fonolojia hujihusisha na mfumo wa sauti za lugha, jinsi sauti hizo zinavyofuata mpangilio maalum, jinsi zinavyobadilika kwa mujibu wa mazingira mbalimbali katika mazungumzo ya kawaida ili kukidhi mawasiliano yanayokusudiwa (Lass 1984:262-263). Katika kufanya hivyo, chati ya IPA haiwezi kuepukika kama kizingiti cha mfumo wa fonimu za lugha kote ulimwenguni. Msikiko wa sauti ni kigezo muhimu. Isitoshe, mbinu hii ilitumiwa na wataalam kama vile Polome (1938) kuchunguzia lugha ya Kiswahili na kutoa kauli ambazo hazijatifuliwa hadi sasa.

### 1.8.2 Uundaji wa Chati ya Kileksia

Chambilecho Hyman (1975), lugha mbili huweza kuwa na mfumo sawa wa kifonetiki lakini zitofautiane kifonolojia. Hivyo basi, msamiati wakilishi ulikusanywa katika nyanja mbalimbali za maisha ya Wanyala (K) - uhusiano wa kijamaa, majina ya sehemu za mwili,

mila, utamaduni n.k. - kwa madhumuni ya kubainisha mifanyiko ya kifonolojia.

### 1.8.3 Kusoma

Ilibidi kujizamisha katika kusoma kazi mbalimbali kama mwongozo katika kutoa kauli mahsusi ambazo zina uhusiano na umuhimu mkubwa na hali zozote zile zinazohusiana na somo hili.

### 1.8.4 Uchunguzi Shiriki

Kujishirikisha katika maongezi ilikuwa mbinu muhimu kwa sababu baadhi ya mifanyiko hudhihirika kwenye vipashio vikubwa kama vile sentensi bali si fonimu au leksia tu. Fauka ya hayo, baadhi ya mifanyiko hudhihirika katika uzungumzi unaoendelea.

Licha ya kwamba hizo ndizo mbinu mahsusi zilizotumiwa, kwanza, ilibidi kutafuta mbinu za kuwateua washiriki waliotumiwa katika utafiti huu. Maadam utafiti huu ni wa kuchunguza mifanyiko ya kifonolojia katika lugha maalum, ambayo haijapitia maandishi, ulichunguza watu mitaani, vijijini, nyumbani na maeneo mengine yaliyoweza kuchangia katika kufanikisha utafiti huu. Uteuzi wenyewe, haswa, ulifanywa kinasibu. Kila mmoja alikuwa na nafasi sawa ya kuteuliwa kushiriki katika utafiti huu. Walakini, katika uteuzi, ilihakikishwa kwamba washiriki wasiopungua hamsini toka maeneo yote waishiko Wanyala (K) walipatikana ili idadi wakilishi ya Wanyala wote kokote waliko katika Wilaya ya Kakamega ipatikane.

Kinachorejelewa hapa ni kwamba uchunguzi huu ulijiingiza kote

kunakoongewa Kinyala (K) na, pia, kujaribu, iwezekanavyo, kutafuta wavyele kokote kule walikokuwa. Ni kutokana na uteuzi nasibu ambapo utafiti ulisababisha kujiingiza vitongojini na kuzungumza na wahusika.

Deta iliyopatikana ilirekodiwa kwenye kanda za kunasia sauti ambazo, baadaye, zilichambuliwa ili kutoa habari iliyotakikana. Fauka ya hayo, baadhi ya mambo yalinakiliwa katika kadi maalum zilizotayarishwa na, pia, kunaswa katika kanda za kunasia sauti.

### 1.8.5 Uchanganuzi wa Deta

Ujuzi na uwezo wa watafiti kama waongeaji asilia wa lahaja hii ulitumiwa kama ithibati nyongeza kwa mambo yaliyojitokeza katika takwimu zilizopatikana kutokana na chati maalum za fonetiki zilizokuwa zimetengezwa. Deta, hata hivyo, zilichanganuliwa kwa njia ya maelezo kufuatia takwimu zilizopatikana.

## 1.9 MAELEZO YA ISTILAHI

Waluyia: Makundi mbalimbali ya watu waishio magharibi mwa Kenya, hususan, wilayani Kakamega, Bungoma, Busia na Vihiga ambao huongea lugha ya Kibantu ijulikanayo kama Kiluyia.

Wanyala: Kundi la watu waongeao mojawapo ya lahaja za Kiluyia ijulikanayo kama Kinyala, ambacho kimegawika mara mbili: Kinyala cha Kakamega (Kinyala K) na Kinyala cha Busia (Kinyala B).

Mifanyiko: Mabadiliko yanayotokea katika kuelekea kubadilisha sifa au sauti za lugha.

Sheria: Kanuni au kaida zinazoongoza mchakato au kitendo fulani.

# SURA YA PILI

# YALIYOANDIKWA KUHUSU SOMO HILI

## 2.0 UTANGULIZI

Katika upekuzi wa vitabu na majarida mbalimbali, hakika haikuwezekana kuona maandishi yoyote yanayozungumzia, moja kwa moja, au hata kwa mbali, mifanyiko ya kifonolojia katika Kinyala (K) mbali na lugha yenyewe kwa jumla. Kinachorejelewa hapa ni kwamba, swala hili halijashughulikiwa katika muktadha lilioshughulikiwa.

Hata hivyo, kuhusu mifanyiko ya kifonolojia katika lugha nyinginezo, kuna maandishi si haba.

## 2.1 YALIYOANDIKWA KUHUSU SOMO HILI

Schane (1972), akiongea juu ya kanuni asilia zinazoambatana na mifanyiko ya kifonolojia, ameziainisha kanuni hizo katika makundi manne kama: wiano, ambapo vitamkwa hufanana kwa kiasi au kikamilifu kutokana na kukaribiana; muundo wa silabi, ambapo kuna mabadiliko katika mgawo wa konsonanti na vokali; kudhoofika na kupata nguvu, ambapo vitamkwa hurekebishwa kulingana na nafasi yake katika neno; na usawazisho changamano, ambapo vitamkwa huungana pamoja katika mazingira fulani.

Anasema kwamba wiano hutoa mifano wazi sana ya kanuni za kiasili. Vipandesauti hupitia mabadiliko ili kukubaliana na sifa fulani za vipandesauti vinavyokurubiana navyo k.m.

i) $$\begin{array}{c}V\\ [-\text{ Nasali}]\end{array} \longrightarrow \begin{array}{c}K\\ [+\text{ Nasali}]/\ [+\text{ Nasali}]\end{array}$$

ii) $$\begin{array}{c}K\\ [-\text{ Ghuna}]\end{array} \longrightarrow [+\text{ Ghuna}]/\ V - V$$

Kinachosemwa hapa ni kwamba vokali ambayo si nasali au konsonanti isiyo ghuna hunasalishwa au kughunishwa baada ya konsonanti ya king'ong'o au kativokali, katika mkondo huo. Katika wiano pamwe wa nasali, kipandesauti huwiana kwenye mahali pa kutamkia kipandesauti kinachofuata. Kwa mfano:

nuna "nyonya"
ŋgona "ninalala"
muma "mbegu/tembe"

Kanuni hapa, ambayo inahusisha alfa ni:

$$[+\text{ Nasali}] \longrightarrow [\alpha\text{ Mahali}]/\ \begin{array}{c}K\\ [\alpha\text{Mahali}]\end{array}$$

Kuhusu ukaakaishaji, Schane (1972) anasema kwamba sauti za koromeo hukaakaishwa katika mazingira ya kabla ya konsonanti ya kaakaa.

$$\begin{array}{c}K\\ [+\text{ Konsonanti}]\end{array} \longrightarrow [+\text{ Kaakaa}]/\ ___\ \begin{array}{c}K\\ [+\text{ Kaakaa}]\end{array}$$

Kundi la pili alilozungumzia Schane ni lile la muundo bora wa silabi. Asema kuwa, kiasili, muundo bora wa silabi ni ule ulio na silabi wazi ya konsonanti na vokali (KV). Vipandesauti, katika lugha, huweza kudondosha au kuchopeka fonimu ili kuvunja mfuatano unaoweza kuzua silabi changamano au tatasi. Kuhusu udondoshi wa konsonanti, mwanaismu huyu anatoa mfano kutoka Kifaransa na kusema kuwa, katika Kifaransa, maneno huishia kwa konsonanti. Walakini, aghalabu, konsonanti hii ya mwisho hudondoshwa ikiwa neno linalofuata huanza kwa konsonanti. Matokeo ni kwamba, kunapata muundo wa silabi unaopendelewa zaidi wa KV, kama vile katika:

| | |
|---|---|
| /pətit ami/ | "rafiki mdogo" |
| /pəti garso/ | "mvulana mdogo" |

Kuhusu udondoshaji wa vokali, anarejelea tena Kifaransa na kusema kuwa vokali katika kibainisho dhahiri /le/ au /la/ hudondoshwa ikiwa neno linalofuata huanza kwa vokali. Udondoshi huu huzuia vokali mbili kuja pamoja:

| | |
|---|---|
| /le garso/ | "mvulana" |
| /l$^{e}$ami/ | "rafiki wa kiume" |
| /l$^{a}$ami/ | "rafiki wa kike" |

Uchopekaji wa konsonanti hutokea katika lugha ya Kihanunoo, inayoongewa kusini mwa Pacific, ambapo konsonanti [h], sana sana, huchopekwa ili kuvunja mlolongo wa vokali, kama vile ilivyo katika:

ʔusa "moja" ʔusahi "fanya iwe moja"

tulu "tatu" tuluhi "fanya iwe tatu"

Anaongeza kuwa uchopekaji katika Kiingereza hutokea katika baadhi ya lahaja zake ambapo [r] huchopekwa pale ambapo neno linaloishia kwa schwa yaani /ə/ linafuatwa na neno linaloanza kwa vokali k.m.

The idea is good ⟶ /θi aidiərz gud/

Uchopekaji wa vokali hutokea katika lugha ya Kilatini na kwamba, katika lugha hii, ni mazoea kwamba maneno hayaishii kwa konsonanti - mlolongo wa kitambaza /l/ na kimadede /r/. Katika hali kama hii, vokali [e] huchopekwa ili kuvunja mlolongo huu wa konsonanti /t/ ikifuatwa na kimadede /r/:

patris "baba" ⟶ pater "baba"

Kuhusu muungano wa konsonanti, anatoa mfano kutoka Kikorea kwa kusema kuwa iwapo kitamkwa ambacho si kifulizwa kitatokea na [h] kisanjari, hubadilishwa na kitamkwa cha mpumuo ambacho si kifulizwa:

nak "anguka" + hwa "ua"

$nak^hwa$ "ua lililoanguka"

kup "inama" + hita "kiambisho tamati kisababishi"

$kup^hita$ "kuinama"

Muungano wa vokali hunatokana katika lugha za kutoka Roma kama vile Kilatini. Katika Kilatini, vokaliunganifu /ai/ na /au/ zuligeuka na kuwa e na o. Maadam mlolongo wa vokali katika lugha hizi umepunguzwa na kuwa vokali moja, muundo wa silabi unaotokea ni rahisi:

| Kilatini | Kiispania | |
|---|---|---|
| kausa | kosa | "kitu" |
| aik$^w$alem | equal | "sawa" |

Akichukua Kiispania kama mfano, anasema kuwa vokali /ɛ/ huongezwa kwa vipandesauti ambavyo huanza na s k.m. -spana linakuwa ɛspana:

Kanuni hapa ni:

$$\# \emptyset \longrightarrow \varepsilon / __ \; sK$$

Mfano huu, licha ya kuwa hauvunji mlolongo wa konsonanti, unachangia katika kueleza dhana ya muundo wa silabi unaopendelewa zaidi ya ule wa kwanza wa KKVKV.

Inaweza kujadiliwa kwamba mlolongo wa vokali unaweza kuvunjwa na uyeyushaji. Hata hivyo, uyeyushaji huweza kuchukuliwa kama mchakato wa muundo wa silabi unaopendelewa sana ingawa, katika baadhi ya lugha, muundo wa silabi unaopendelewa zaidi haufikiwi kabisa. Schane anaweza kulijadili swala hili kuwa huu ni mfumo kingazi katika michakato ya muundo wa silabi. Katika michakato

ya aina hii, muundo wa Konsonanti-Kiyeyusho-Vokali-Kiyeyusho-Vokali au Konsonanti-Kiyeyusho-Vokali-Konsonanti-Vokali-Konsonanti unapendelewa zaidi ya KKVKV n.k. kama vile katika lugha ya Kinandi:

| | | |
|---|---|---|
| ko + a + we /ko + o + we/ | [kwowe] | "nilienda" |
| ma + ki + am /makiam/ | [makjam] | "nilimpata" |

Hali hii ya mpangilio kihadhi, pia, inapatikana katika Chomsky na Halle (1968) katika hali dhihirishi. Silabi inayopendelewa sana huhusisha udondoshaji wa vokali kabla ya vokali nyingine, uchopekaji wa vokali, na muungano wa vokali, kama vile ilivyoelezwa hapo juu.

Kundi jingine alilozungumzia ni lile la ubainishi wa hali ya juu. Dhana hii ilijadiliwa na Trubetskoy (1939), Jacobson (1940) na Martinet (1955). Pia, inapatikana katika Chomsky na Halle (1968) katika hali dhihirishi. Katika hali kama hii, vipandesauti huonekana kutoafikiana (kutofanana) kabisa. Anatoa mfano wa mfumo wa vokali tatu ambapo tunaweza kukisia kuwa katika mfumo huo, tunatarajia vokali (asilia) kuwa /i/, /a/, /u/ kwa sababu zinawakilisha sehemu za mwisho kabisa za kila upande wa chati ya vokali. Vokali za juu zinakinzana au kutofautiana sana na zile za chini, tofauti na /e/, /ɑ/, /o/ ambapo vokali kati zinatofautiana na zile za chini.

Schane anashikilia pia kwamba hali ambapo usawazisho changamano unatokea si kwa njia ya usilimisho bali kwa ajili ya kanuni za

ukinzani wa hali ya juu. Anasema kwamba katika Kiingereza na Kijerumani, kuna usawazisho wa vokali legevu katika silabi wazi ya mwisho, ambapo vokali ni kaze k.m.

**Kiingereza**

I am ⟶ I'm

I have ⟶ I've

**Kijerumani**

wie geht es ⟶ wie geht's

Hali hii husababisha kudondoshwa kwa vokali legevu za kiwango cha kadiri zinazokurubiana na vokali kaze au katikati ya konsonanti. Isitoshe, katika Kijerumani, obstruenti huondolewa ughunaji zipatikanapo mwishoni mwa neno. Hii ni hali ya juu ya ubainishi, tofauti na ughunaji ambao ni mfanyiko wa wiano. Schane anafutilia mbali pendekezo kuwa kutoghunisha ni mfano wa wiano ambapo mpaka wa neno unachukuliwa kuwa na sifa [+ Ghuna] au kimya. Anadokeza kuwa mpaka wa neno na konsonanti hudhihirisha sifa sare katika kanuni za kifonolojia, kiasi kwamba inaweza kuchukuliwa kuwa mpaka wa neno yaani #, una sifa [+ Konsonanti]. Hii ni kwa sababu nadharia ya mfumo wa silabi inayopendelewa zaidi hutoa maelezo ya mpaka wa neno au konsonanti kama mazingira badalia ya kanuni moja au sare. Kwa hivyo, mpaka wa neno si lazima uwe na sifa ya kifonolojia bali, katika wiano, kanuni lazima zichukue sifa za kifonolojia za vipandesauti vinavyokurubiana.

Akizungumzia juu ya kundi la nne la kupata nguvu na kudhoofika, Schane anasema kuwa katika vipandesauti, kupata nguvu hutokea kwa msingi wa ngazi za kihadhi kwamba baadhi ya mifanyiko, katika lugha fulani, hudhoofisha au huvipa nguvu vipandesauti. (Walakini, mfanyiko huu waonekana kuwa sehemu ya wiano). Wiano mbele (sinokopi) na wiano nyuma (apokopi) ni matokeo ya udhoofishaji. Katika sinokopi, vokali iliyo karibu na nyingine inayokazwa hudondoshwa; k.m. katika Kiingereza tunapata maneno "happening" na "chocolate" yakitamkika "happ'ning" na "choc'late". Katika apokopi, vokali ya mwisho isiyokazwa hupotezwa kama vile inavyojitokeza katika vokali inayofanana na schwa katika Kifaransa:

fille /fiyə/ ⟶ [fiy]

Licha ya kwamba mchango wa Schane ni mkubwa mno, hauzingatii Kinyala (K) katika ubinafsi wake na, hivyo basi, mchango wake ni kama mwongozo tu wa kufuatwa katika kutolea maelezo ya mifanyiko ya kifonolojia katika Kinyala cha Kakamega.

Hyman (1970, 1973a, 1973b na 1975) amedokeza kwamba kanuni za kifonolojia huzua mambo matano tu, ambayo ni udondoshaji wa kitamkwa k.m. ba+ana ⟶ bana, uchopekaji wa kitamkwa k.m. mai ⟶ maji, ubadilishaji wa kitamkwa ma+ino ⟶ meno, muungano wa vitamkwa k.m. ma+ingi ⟶ mangi, kubadilisha sifa za vitamkwa kama vile unasalishaji k.m /map/ ⟶ /mæ̃p/, ughunaji k.m pakha ⟶ mbakha n.k. Haya yalitokana na madai ya mwanaismu huyu kwamba mgawo wa Schane, wa mifanyiko ya

kifonolojia, unamfanya ajirudierudie zaidi, ndiposa akachukulia kwamba wiano ni udhoofishaji.

Kwa upande wake, Stampe (1979) amejaribu kuainisha nadharia yake ya mifanyiko ya kiarudhi (prosodic processes) kwa kujeleza mifanyiko ya aina mbali mbali. Amezungumzia juu ya toni katika neno, yaani kila kitamkwa kina toni yake - fonolojia ya kiarudhi. Anasema kuwa kuna mifanyiko ya kudhoofisha ambayo hutawaliwa, sana sana, na muktadha na hutokea katika nafasi hafifu ya kiishio au kifungio ya silabi kama vile wiano, udondoshaji n.k. Anaongeza kuwa mifanyiko ya kupata nguvu hutokea katika sehemu ya mwanzo/kitangulizi ya silabi, kama vile, usigano, uchopekaji, uhamishi wa vokali n.k. - ingawa si zote. Stampe hakutaka kujirudiarudia kama Schane.

Crowley (1992) anatoa madai kuwa si ajabu kuona kwamba lugha zote hubadilika kuzingatia mapito ya nyakati na kwamba inaweza kustaajabisha kuona kwamba lugha tofauti huonekana kubadilika katika njia zinazokaribiana. Anatoa mfano wa sauti [s] katika Kiurdhi (Urdhi) ambayo, anaendelea kudai, imepitia mabadiliko na kuwa [w] katika lugha ya sasa.

Katika insha yake, Fairbanks (1973), amesema kwamba, licha ya kuwa mengi yameandikwa kuhusu fonolojia zalishi mapisi (generative historical phonology), kuna mengi yaliyoachwa ya kutamaniwa. Anadokeza kuwa kuna mparakanyiko unaoletwa na uainishi kati ya mifanyiko ya mabadiliko na matokeo ya mifanyiko hiyo kwa lugha jinsi inavyochanganuliwa na wanaismu. Mwanzoni,

wanafonimiki waliongea juu ya mabadiliko ya fonimu kana kwamba ni mfanyiko wa mabadiliko. Hill (1936) anayapa uzito mawazo haya kwa kusema kuwa mabadiliko hayo yanaweza kuathiri muundo wa kifonimiki na sarufi ya lugha kama vile ilivyochanganuliwa na wanauzalishi.

Yaonekana kwamba wanauzalishia walijishughulisha sana na mabadiliko ya kisinkronia kuliko dayakronia. Tunapotaka kuelewa vyema historia ya lugha, ni muhimu kuzingatia kanuni za kisinkronia na kidayakronia kwa sababu, kanuni za kidayakronia ni kiwakilishi cha michakato ya mabadiliko katika lugha; na, mabadiliko katika kanuni za kisinkronia ndiyo matokeo ya michakato hii. Kutokana na yale yaliyosemwa hapo juu, maandishi yaliyorejelewa ni ya kinadharia. Hata hivyo, kuna baadhi ya wataalam ambao wamejaribu kuzingatia lugha binafsi mbalimbali.

Katika tasnifu zao za shahada ya uzamifu, Bakari (1982) na Maganga (1990) wanaishughulikia mofofonolojia ya lugha ya Kiswahili. Ambapo Bakari anazichunguza lahaja zote za Kiswahili zisemwazo Kenya, Maganga alizishughulikia Kiswahili Sanifu, Kipemba, Kitumbatu na Kimakunduchi. Ingawa kazi hizi hazikushughulikia Kinyala (K), moja kwa moja, zinachangia pakubwa katika uibuaji wa mfumo wa kifonolojia wa Kinyala na mjadala kuhusu taratibu za kanuni za kifonolojia na kimofofonolojia, si kwa Kiswahili tu bali kwa Kinyala (K) ambacho kinawekwa katika kundi moja na Kiswahili - Kibantu. Kanuni na taratibu hizi hujitokeza kila mara katika mazingira husika ya kimuundo.

Ball (1971) amechunguza, kifonolojia, tofauti zipatikanazo katika wiano wa maneno ya mkopo yanayotokana na Kiarabu na Kiingereza katika Kimvita. Tofauti hizi zinaelezeka kwa kupanga kanuni katika viwango viwili vya makisio. Matokeo ya jumla ni kwamba kunazuka ujumlishaji kiholela wa kanuni kama ionekanavyo katika mifano ifuatayo:

nafasi ya /q/ inachukuliwa na /k/ k.m.

Qahari → Kahari

" " /gh/ " " /g/

au inapoteza ughunaji na kuwa /x/ k.m.

ghafla → [gafla]

lugha → [luga]

agh → [aX]

Uchanganuzi wa aina hii, katika uchunguzi-leo, hauwezi kuchukuliwa kama uchanganuzi wa kiisimu; yafaa uonyeshe mahali au mazingira yanayosababisha mabadiliko haya.

Akiongea juu ya fonolojia ya silabi za Kiswahili Sanifu na za Kimarama, katika tasnifu yake ya M.Phil., Aswani (1993) amedokeza kuwa muundo wa kiisimu wa lugha husababisha vipashio vinavyoweza kuifanyiza silabi. Muundo huo huelekeza mfuatano wa vipashio husika. Katika hali hii, mwanaismu huyu ameichunguza silabi ya Kimarama kifonetiki na kifonolojia. Anadai kuwa fonetiki inatuwezesha kuibaini silabi kama tamko, na fonolojia ikatupelekea kuchunguza sauti mbalimbali zinazopatikana katika

lugha, na jinsi zinavyoungana kufanyiza vipashio vikubwa zaidi kama silabi na neno.

Kutokana na uchunguzi wa Aswani kuhusu silabi ya Kiswahii Sanifu na ya Kimarama, tunakutana na uchunguzi ambao, licha ya kwamba haurejelei mifanyiko ya kifonolojia katika ukamilifu wake, umetupa mchango mkubwa sana wa kuweza kuchunguza lugha ya Kinyala (K), ambayo awali ilichukuliwa kuwa katika kundi moja na Kimarama - Kiluyia. Isitoshe, muundo wa silabi ni jambo muhimu sana, na huchukuliwa kama mojawapo ya mifanyiko ya kifonolojia.

De Blois (1975) na Kasaya (1992) wameshughulikia fonolojia ya lahaja kadhaa za Kiluyia. Ambapo De Blois ameshughulikia fonolojia zalishi ya Kibukusu na sehemu fulani za muundo wa Kibantu, Kasaya amejihusisha na uchunguzi wa mifanyiko mikuu inayodhihirika katika Kilogoli, Kiwanga na Kibukusu, ambazo ni baadhi ya lahaja za Kiluyia, ambacho kilihusisha Kinyala wakati fulani. Ingawa kazi zao zinatoa mchango mkubwa kwa utafiti wetu, kazi hizi hazikujihusisha na lahaja ya Kinyala (K). Maadam lugha zinaweza kuwa na mfumo sawa wa kifonetiki na fonolojia itofautiane, ni muhimu kwamba lahaja ya Kinyala (K) ichunguzwe kama lahaja mahsusi ya Kinyala, lugha iliyovyazwa na Kiluyia.

Lass (1984) amedai kwamba dhana zinazorejelea mifanyiko huweza kuelezeka, kwa kadiri, tunapozingatia uhusiano kati ya utoaji na upokeaji ambao ni wa muda mfupi, katika kueleza mabadiliko ya kihistoria. Anaorodhesha mifanyiko ya kifonolojia inayotokea katika lugha za ulimwengu kama wiano, kudhoofika na kupata nguvu,

miundo ya silabi, usawazisho changamano, tabdili, usigano, haplolojia na sandhi.

Walakini, kama ilivyodokeza hapo awali, lahaja ya Kinyala (K) haijatendewa haki kiisimu na, hivyo basi, maandishi hayo yote ni mwongozo tu usiokuwa na chochote, hakika, kuhusu Kinyala (K) kama lugha mahsusi.

## 2.2 HITIMISHO

Kijumla, maandishi haya yalitoa mwanga hasa kwa upande wa mbinu za kufanya utafiti na vigezo muhimu vya kuzingatia katika uchunguzi wa lugha kama huu. Matatizo ambayo wataalam hawa walikumbana nayo ni kijulisho mapema cha baadhi ya matatizo ambayo mtafiti anaweza kukumbana nayo na, hivyo basi, kuwezesha kutafuta njia za kuepuka matatizo kama hayo.


# SURA YA TATU

# SAUTI ZA KINYALA CHA KAKAMEGA

## 3.0 UTANGULIZI

Lugha huundwa kwa sauti. Ili kuelewa asili ya lugha, ni lazima tuanze kwa kuangalia sauti zake. Uchunguzi wa sauti, kwa hivyo, ni muhimu kiismu kuliko ule wa maandishi au viashiria. Anachozingatia sana mwanaismu ni sauti ambazo hutolewa na ala za matamshi za mwanadamu. Mwanda wa kiismu unaojishughulisha na uchunguzi wa sifa za sauti unajulikana kama fonetiki. Chambilecho Mario Pei (1965:11) fonolojia ni uchunguzi wa sauti za lugha vile zinavyobadilika na kugeuzaumbo katika maendeleo ya lugha, na fonetiki ndiyo sayansi, uchunguzi, uchanganuzi na utabakishaji wa sauti za lugha bila kurejelea maendeleo yake kihistoria, lakini kwa kurejelea utoaji, uenezaji na upokeaji wake. Kinachojitokeza hapa ni kwamba fonolojia na fonetiki huchangiana, kiasi kwamba ni vigumu kuzungumzia fonolojia bila kurejelea fonetiki. Isitoshe, yafaa tuzingatie kwamba istilahi tutakazozingatia, kiismu, kuelezea sauti za Kinyala (K) zitajikita katika fonetiki tamkaji bali si fonetiki msikiko au fonetiki akostika. Kwa hivyo, ili tuweze kushughulikia sauti za Kinyala (K), ni muhimu tuelewe ala zitumiwazo na mwanadamu katika utoaji wa sauti. Kwanza, tuutazame mchoro:

<u>Mchoro 1: Ala za Sauti</u>




1. Midomo 2. Meno 3. Ufizi 4. Kaakaa ngumu
5. Kaakaa laini 6. Koromeo 7. Ncha ya ulimi
8. Lamina 9. Nyuma ya ulimi 10. Umio wa hewa/chakula
11. Nyuzi za sauti

### 3.0.1 ALA ZA SAUTI

Kimsingi, ala za sauti hutenda kazi nyinginezo kisayansi. Kwa hivyo, kazi hizi haziambatani na utoaji wa sauti. Kwa mfano, mapafu husafisha oksijeni kwa damu ilhali nyuzi za sauti, zinapovutwa pamoja, hufunga umio wa hewa ili kuzuia chakula kwenda njia isiyotakikana. Vile vile, nyuzi za sauti husaidia wakati wa kukohoa, kwa mfano, kuelekeza chakula kutakikanako.

Ulimi na meno, kwa upande wake, husaidia wakati wa kula na, hivyo basi, kazi nyinginezo za ala hizi hazipaswi kuleta mparakanyiko. Mkondo utokao kwenye mapafu kuelekea mdomo na pua, ambamo hewa kutoka mapafuni hupitia, huitwa mkondohewa. Mkondo huu una pango la mdomo na pango la pua. Ala zipatikanazo katika pango la mdomo ni mdomo wa chini na ulimi. Ulimi umegawanywa katika sehemu tano ambazo ni ncha, lamina, sehemu ya mbele, sehemu ya nyuma na mzizi. Ncha ya ulimi ni ile sehemu ya mbele kabisa ambayo huitwa kilele. Lamina, ambayo huitwa sehemu ya kati, hupatikana baada ya ncha ya ulimi. Sehemu ya mbele huwa upande wa chini wa kaakaa ngumu na sehemu ya nyuma huwa chini ya paa la mdomo (kaakaa laini). Mzizi wa ulimi huwa chini katika sehemu ya juu ya koromeo.

Sehemu ya juu ya mkondohewa huwa na mdomo wa juu, meno ya juu, ufizi, kaakaa ngumu, kaakaa laini, na ukuta wa nyuma, ambao ni sehemu ya mkondohewa kati ya koromeo na nyuzi za sauti.

Mifumo mitatu ya viungo vya mwili hushiriki katika utoaji wa sauti, ambavyo ni pumzi, fona na utamkaji.

### 3.0.2 PUMZI

Pumzi hupatikana kifuani na huhusisha mapafu na misuli, ambayo husaidia kufungua na kubana mapafu. Mfumo huu ndio wa kwanza kabisa katika utoaji wa sauti maadam unahusisha pumzi inayoranda au kutembea au kuenea.

### 3.0.3 FONA


Fona hupatikana kooni na huhusisha nyuzi za sauti. Sehemu yake ya mbele huonekana waziwazi kwa wanaume watu wazima.

### 3.0.4 UTAMKAJI

Utamkaji hutendeka kichwani, na huhusisha pua, midomo, kinywa na viungo vyake kama meno na ulimi. Ingawa pumzi inayoenea ni muhimu kwa utoaji wa sauti, kuna kitu kingine muhimu, pia. Pumzi inayoenea ili kutoa sauti lazima ifanyiwe marekebisho ili sauti, zinazoweza kusikika zitolewe; na ni mfumo fona na mfumo tamkaji ambayo huingilia kati ya pumzi inayotolewa, katika utoaji wa sauti. Ithibati inatolewa na ukweli kwamba, aghalabu, sauti hutolewa kwa marekebisho ya mkondohewa ambao hutolewa kwenye mapafu kuelekea pango la kinywa, kupitia glota na mkondohewa. Katika nyuzi za sauti, kuna nafasi laini zinazotenganisha nyuzi zenyewe. Sauti tunazotoa hutegemea jinsi utoaji wa pumzi kutoka mapafu unavyoingiliwa na mfumo fona na mfumo tamkaji.

Lugha yoyote ile huwa na mpangilio maalum wa sauti, ambao huitwa mfumo wa sauti. Kinyala (K) kina sauti nyingi, konsonanti na vokali pia. Sawa na lugha nyingine za Kiafrika, Kinyala (K) hudhihirisha mshabaha mkubwa kati ya lugha andishi na ile ya

kuzungumza. Kila lugha hutumia alama ambazo huzingatia mfumo wa Utamkaji Pokezi (UP), ambao unajulikana kwa Kimombo kama <u>Received Pronunciation</u> (RP). Sauti ambazo hutofautisha neno na jingine huchukuliwa kuwa na maana. Mfano ni /l/ na /r/, ambazo hutusaida kutofautisha kati ya "lia" (kula) na "ria" (ogopa). Lugha huundwa kwa sauti ndogo sana ziitwazo fonimu, ambazo tutazieleza katika makala haya. Fonimu zikisimama pekee huwa hazina maana. Zinaungana kuunda mofimu ambazo huunda neno. Maneno huunda kifungu na vifungu huunda sentensi:




Ingawa kila lugha ina ruwaza ya kipekee ya mpangilio wa sauti, sauti za lugha zote hutabakishwa katika makundi mawili, ambayo ni konsonanti na vokali.

### 3.1 KONSONANTI ZA KINYALA (K)

Fonolojia ya Kinyala (K) si pana sana. Hata hivyo, ni muhimu tuelewe kwamba konsonanti huelezwa kwa kuzingatia sifa tatu kuu, ambazo ni: upumuaji, mahali pa kutamkia na jinsi ya kutamka. Hata

hivyo, hebu kwanza tuchunguze mwingilio wa pumzi inayoenea na mfumo wa fona, ambao huelekeza sauti kuelezwa kama hafifu au ghuna.

**a) HALI YA GLOTA**

Pumzi zinazotoka mapafuni husukumwa nje kupitia mkondohewa kuelekea nyuzi za sauti na kupitia kinywani, puani au viungo vyote viwili. Katika sehemu ya nyuzi za sauti, kuna viungo vyororo ambavyo hujenga nyusi hizo. Viungo hivyo huweza kuchukua hali mbili: vinaweza kupanuka au vinaweza kubana. Ikiwa nyuzi za sauti zimepanuka, mwanya huachwa katikati, na ikiwa zimebanwa huwa, katika hali fulani, zimefungwa. Hali hii husababisha glota kutoa sauti zinazotofautiana.

Glota inaweza kufunguka na, inapofunguka, pumzi husukumwa juu ya mapafu kupitia mkondohewa uliobanwa. Sauti zote, ambazo hutolewa wakati ambapo glota imefunguka, huitwa sauti hafifu. Ikiwa nyuzi za sauti zimevutwa pamoja, glota hufungika na pumzi kutoka mapafuni, sana sana, husukuma nyuzi hizo ili kuzitenganisha na kusababisha msepetuko. Sauti zitolewazo katika hali hii huelezwa kuwa ghuna. Deta ifuatayo itatoa mwangaza kwa maelezo hayo:

| **A** | **B** |
|---|---|
| <u>Sauti Hafifu (H)</u> | <u>Sauti Ghuna (Gh)</u> |
| /t/ k.m. taa "chota/taa" | /d/ k.m. ndusa "ninatapika" |
| tema "jaribu" | ndema "ninajaribu" |

| | | | |
|---|---|---|---|
| /f/ k.m. | fwala "vaa"<br>fwana "fanana" | /v/ k.m. | vecha "fyeka"<br>vikha "weka" |
| /p/ k.m. | para "fikiri"<br>pima "pima" | /b/ k.m. | mbara "ninafikiri"<br>mbima "ninapima" |
| /k/ k.m. | kama "ongeza"<br>koma "toroka" | /g/ k.m. | ngama "ninaongeza"<br>ngoma "ninatoroka" |

Kuna hali nyinginezo ambazo huweza kuchukuliwa na glota mbali na kufunguka na kusepetuka. Hali hizo ni kama vile kupunguzwa kwa upana na kufunguka kabisa. Ikiwa glota imepunguzwa upana, nyuzi za sauti huvutwa karibu lakini si karibu sana kiasi cha kuweza kusababisha msepetuko. Kuja karibu kunapunguza upana wa glota tu, hali ambayo huzuia pumzi kutoka mapafuni, hivyo kutoa sauti ya mnong'ono. Sauti yoyote inayotolewa ikiwa glota imepunguzwa upana huwa ni mnong'ono. Ikiwa glota imefungika kabisa, nyuzi za sauti hukurubiana kabisa na kushikana na, hivyo, kuzuia pumzi kupita. Glota huwa katika hali hii kwa vitendo visivyo vya kiismu kama vile wakati tunapokohoa.

**b) MAHALI PA KUTAMKIA**

Katika utoaji wa konsonanti, pumzi hupitia pango la kinywa ambapo, kwa kiasi fulani, huzuiwa. Mahali ambapo pumzi huzuiliwa, wakati sauti inapotolewa, huitwa mahali pa kutamkia. Mahali pa kutamkia ni muhimu sana katika uelezaji wa sauti, hususan, konsonanti. Maadam tumeshughulikia ala za sauti, ni muhimu, sasa, turejelee sauti na mahali pa kutamkia.

Katika utamkaji wa /p/, mdomo wa chini na ule wa juu hugusana, na pumzi kutoka mapafuni huzuiliwa na midomo. Kwa hivyo, /p/ ni sauti ya midomo. Isitoshe, /b/ hutamkiwa pale pale. Sauti hizi, mbili, basi, ni za midomoni. Tukiangalia /f/, tunaona kuwa mdomo wa chini hukaribia meno ya juu. Pumzi kutoka mapafuni huzuiliwa kati ya mdomo wa chini na meno ya juu. Kwa mintarafu hii, /f/ inakuwa sauti ya mdomo-meno. Mahali pale pale ndipo patamkiwapo /v/. Tukirejelea /t/ na /d/, tunaona kuwa ncha ya ulimi hukaribia ufizi. Pumzi kutoka mapafuni huzuiliwa kati ya ala hizi mbili. Kwa msingi huu basi, /t/ na /d/ zinakuwa sauti za ufizi.

Tukizingatia hali ya glota na mahali pa kutamkia, tunaweza, kwa hivyo, kueleza jozi hizi za sauti ifuatavyo:

/p/ sauti hafifu ya midomoni

/b/ sauti ghuna ya midomoni

/f/ sauti hafifu ya mdomo-meno

/v/ sauti ghuna ya mdomo-meno

/t/ sauti hafifu ya ufizi

/d/ sauti ghuna ya ufizi

Sauti /p/ na /b/, /f/ na /v/ na /t/ na /d/ huelezwa kuzingatia vigezo vitatu ambavyo ni hali ya glota, mahali pa kutamkia na jinsi ya kuzitamka. Sauti /p/ na /b/, ni za midomoni na, vile vile, vituo. Hata hivyo, vituo hivi vinatofautiana kwa sababu /p/ ni kituo hafifu cha midomoni ilhali /b/ ni kituo ghuna cha midomoni. Tunachosema hapa ni kwamba, katika utamkaji wa /p/, /f/ na /t/, nyuzi za sauti hufunguka na, hivyo, zote ni sauti hafifu.

Ambapo /p/ ni kituo hafifu cha midomoni, /f/ ni kikwaruzo hafifu cha mdomo-meno na /t/ ni kituo hafifu cha ufizi. Sauti /b/, /v/ na /d/ zinatofautiana na /p/, /f/ na /d/ kwa sababu ni ghuna. Hata hivyo, kabla ya kuingilia suala la jinsi ya utamkaji, ingekuwa bora tutazame mahali penginepo pa kutamkia.

Tunapotamka sauti /tʃ/ na /ɟ/, tuhaona ala mbili zikishiriki, ambazo ni ncha ya ulimi, ambayo hukaribia kaakaa ngumu, ilhali sehemu ya mbele ya ulimi hujipinda kwenye ukuta wa kinywa. Sauti hizi hutokea katika maneno kama:

chekha - /tʃeXa/ "cheka"

njekha - /ɲɟeXa/ "ninacheka"

chula - /tʃula/ "toka"

njula - /ɲɟula/ "ninatoka"

chola - /tʃola/ "dondoa"

njola - /ɲɟola/ "ninadondoa"

Sauti nyingine zipatikanazo kwenye kaakaa ngumu ni kama vile /ɲ / na /j/ kama vile zinavyodhihirika katika maneno yafuatayo:

nyama - /ɲama/ "nyama"

nyuma - /ɲuma/ "nyuma"

nyala - /ɲala/ "ninaweza"

nywa - /ɲwa/ "ninakunywa"

yola - /jola/ "fika"

yenya - /jeɲa/ "taka"

yova - /jova/ "changamka au kuwa chonjo"

Kuhusu sauti za kaakaa laini, sehemu ya nyuma ya ulimi hukaribia kaakaa laini. Sauti zitamkiwazo kwenye kaakaa laini ni:

| | |
|---|---|
| /k/ kama vile katika | kania - /kania/ "kataza" |
| | kama - /kama/ "ongeza" |
| | khaka - /Xaka/ "jaribu" |
| | kukhu - /kuXu/ "nyanya" |
| /g/ kama vile katika | nga - /ŋga/ "kama" |
| | ngona - /ŋgona/ "ninalala" |
| | ngava - /ŋgava/ "ninagawa" |
| | ngania - /ŋgania/ "ninakataza" |
| | ngama - /ŋgama/ "ninaongeza" |
| /ŋ/ kama vile katika | ng'asa - /ŋasa/ "enea" |
| | ng'ala - /ŋala/ "kusudia" |
| | ng'ombe - /ŋoŋbe/ "ng'ombe" |

Kwa upande wake, sauti ya koromeo ni moja tu, ambayo ni /h/, kama vile katika:

hera - /hera/ "pumua"

heya - /heja/ "fanya uasherati"

## c) JINSI YA KUTAMKA

### Vituo

Kwa hali fulani, vituo hutengwa katika makundi mawili kama vipasuo na vizuio-kwamiza. Vipasuo ni sauti ambazo hutolewa wakati ambapo ala za kutamkia hukutanishwa na kukusanya pumzi.

Pumzi hiyo husababisha ala hizo kutenganishwa ghafula kana kwamba kuna mpasuko. Baada ya kutenganishwa kwa ghafula, sauti zinazotoka hutoka kwa nguvu. Sauti hizo ndizo zijulikanazo kama vipasuo, yaani kuna mpasuko. Licha ya kwamba sauti hizo ni vituo, ni heri zipambanuliwe hivi kwa kupewa jina jingine la vizuio ili kuzitenganisha na vizuio-kwamiza. Kuna vipasuo vya aina mbili vile vile, ambavyo ni hafifu na ghuna, kama vile ilivyo hapa chini:

| | Midomo | Ufizi | Kaakaa laini |
|---|---|---|---|
| Hafifu | p | t | k |
| Ghuna | b | d | g |

Vizuio-kwamiza, kwa upande wake, huitwa hivyo kwa sababu, wakati wa kuzitamka sauti hizi, pumzi huzuiliwa na ulimi pamoja na kaakaa ngumu. Zinapotoka, hutoka kwa shida ndipo zikaonekana kuwa ni za kukwamiza. Konsonanti za vizuio-kwamiza ni /tʃ/ na / ɟ / ambapo /tʃ/ ni hafifu na / ɟ / ni ghuna.

**Vikwaruzo/Vikwamizo**

Vikwaruzo, ambavyo pia huitwa vikwamizo, ni sauti ambazo, wakati wa kuzitamka, pumzi hutoka kwa kukwaruzana au kukwamizwa na ulimi pamoja na zile ala nyingine zinazotumika kuzitamkia. Ala hizi huwa zimekaribiana na pumzi hupitishwa kati yake. Zifuatazo ndizo sauti za vikwaruzo katika Kinyala (K):

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Midomo | Mdomo-Meno | Ufizi | Kaakaa laini | Koromeo |
| H | f | s | X | h |
| Gh | v | | | |

**Nazali**

Konsonanti za nazali, ambazo pia huitwa vipua au ving'ong'o, hutamkwa kwa kukutanisha ala za sauti ambapo kilimi hufunga pango la kinywa na, hivyo, pumzi nyingi hutokea kwenye pua. Sauti zote za nasali hutamkwa kwa mghuno. Sauti hizo ni:

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Midomo | Midomo-Meno | Ufizi | Kaakaa ngumu | Kaakaa laini |
| m | ɱ | ɲ | n | |

Ni muhimu ieleweke kwamba /ɱ/ ambayo ni nazali ya midomo-meno hutokea tu pale ambapo nazali /m/ ya midomoni hufuatwa na kituo cha midomo.

**Kitambaza**

Sauti ya kitambaza, katika Kinyala (K), ni moja tu nayo ni /l/. Wakati wa kuitamka sauti hii, lamina hukutanishwa na ufizi. Ulimi hutambaza pumzi katika pande zote - kushoto na kulia za ulimi. Sauti hii huwa ni hafifu.

**Kimadede**

Utamkaji wa kimadede huhusisha kufungafunga na kufunguafungua. Sauti ya kimadede hutolewa pale ambapo ala inayotetematetema hupigapiga kwenye ala bwete. Kimadede kipatikanacho katika Kinyala (K) ni /r/. Katika utamkaji wa sauti hii, ala

inayotetematetema, ambayo ni ncha ya ulimi, hupigapiga kwa mfululizo kwenye ufizi.

**Vilainisho**

Vilainisho, ambavyo pia huitwa viyeyusho au nusu vokali, hutamkwa wakati ambapo ala zinazohusika hukaribiana na kupunguza upana wa umio wa hewa, lakini si kwa kiwango ambacho huweza kuzua mkwaruzano, kama vile ilivyo katika utoaji wa vikwaruzo. Vialinisho hutamkwa kwa utaratibu mwingi kama vile vokali - bila mkwaruzano au mgusano wa pumzi na ala - ndiposa sauti hizi kuitwa nusu vokali. Vilainisho, ambavyo ni hafifu, vinawakilishwa na:

| Midomo | Kaakaa ngumu |
|---|---|
| w | j |

Mchoro 2. Chati ya Konsonanti za Kinyala (K)

**Mahali pa Kutamkia**

| | | Midomo | Midomo meno | Ufizi | Kaakaa ngumu | Kaakaa laini | Koromeo |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Vipasuo | H | p | | t | | k | |
| | GH | b | | d | | g | |
| Vizuio Kwamiza | H | | | | tʃ | | |
| | GH | | | | dʒ | | |
| Vikwaruzo | H | | f | s | | X | h |
| | GH | β | v | | | | |
| Nasali | H | | | | | | |
| | GH | m | ɱ | n | ɲ | ŋ | |
| Kitambaza | H | | | l | | | |
| | GH | | | | | | |
| Kimadede | H | | | | | | |
| | GH | | | r | | | |
| Vilainisho | H | w | | | j | | |
| | GH | | | | | | |

Kutokana na chati hiyo, tunaona kuwa Kinyala (K) kina sauti ishirini na tatu (23) za konsonanti, ambazo hudhihirika kama ifuatavyo, katika maneno:

/p/ k.m. para /para/ "fikiri"

pukha /puXa/ "kuwa mchafu"

/b/ k.m. mbara /ɱbara/ "ninafikiri"

mbukha /ɱbuXa/ "ninachafuka"

/t/ k.m. takha /taXa/ "taka au tafuta"

techa /tetʃa/ "kinga"

/d/ k.m. ndakha /ndaXa/ "ninataka au ninatafuta"

ndecha /ndetʃa/ "ninakinga"

/k/ k.m. kama /kama/ "ongeza"

kesa /kesa/ "vuna"

/g/ k.m ngama /ŋgama/ "ninaongeza"

ngesa /ŋgesa/ "ninavuna"

/tʃ/ k.m. chia /tʃia/ "enda"

chukha /tʃuXa/ "mwaga"

/ ɟ/ k.m njia /ɲɟia/ "ninaenda"

njukha /ɲɟuXa/ "ninamwaga"

/β / k.m. bana /β ana/ "watoto"

khaba /Xaβ a/ "pingana"

/f/ k.m. fwana /fwana/ "fanana/labda"

fwala /fwala/ "vaa"

/v/ k.m. vikha /viXa/ "weka"

vecha /vetʃa/ "fyeka"

/s/ k.m. sama /sama/ "bweka"

sava /sava/ "omba"

/X/ k.m. khama /Xama/ "kama"

khoma /Xoma/ "gonga k.m. msumari"

/h/ k.m. hano /hano/ "hapa"

hera /hera/ "pumua"

/m/ k.m. mama /mama/ "mama"

mera /mera/ "lewa"

/ɱ/ k.m. mbere /ɱbere/ "changa"

mbekhe /ɱbeXe/ "nibebe

/n/ k.m. nange /naŋge/ "na mimi"

nava /nava/ "shona au vua samaki"

/ɲ/ k.m. nyama /ɲama/ "nyama"

nyala /ɲala/ "ninaweza"

/ŋ/ k.m. ng'ombe /ŋombe/ "ng'ombe"

ng'eng'a /ŋeŋa/ "ramba"

/l/ k.m. lima /lima/ "lima"

luma /luma/ "uma"

/r/ k.m. ria /ria/ "ogopa"

risia /risia/ "kemea k.m. mashetani"

/w/ k.m. wange /waŋge/ "ni wangu"

weya /weja/ "unafagia"

/j/ k.m. yala /jala/ "tandika k.m. matandiko"

yema /jema/ "simama"

Kihistoria, kulikuwa na sauti /ts/ ambayo imepotea na mahali pake kuchukuliwa na /tʃ/ na /ɟ/ kama vile katika:

yitsa ⟶ yicha "njoo"

tsukha ⟶ chukha "mwaga"

ntsia ⟶ njia "ninaenda"

ntsukha ⟶ njukha "ninamwaga"

## 3.2 VOKALI ZA KINYALA (K)

Vigezo vitatu vya kuainishia konsonanti, yaani hali ya glota, mahali pa kutamkia na jinsi ya kutamka, si muhimu katika uelezaji wa vokali. Hii ni kwa sababu, katika utoaji wa vokali, hakuna ala zikurubianazo ili kupunguza upana wa mkondohewa ili kuzuia pumzi. Kwa hivyo, hakuna mkwaruzano au msuguano katika pango la kinywa au kooni, kama vile ilivyo na konsonanti. Isitoshe, ingawa vokali hafifu zinaweza kupatikana, ni nadra mno na, hivyo basi, si swala kuu tunapozingatia Kinyala (K). Tunabakia kujiuliza na kujibu swali: Vokali hutolewaje?

Vokali mbalimbali hutolewa kwa kubadilisha umbo la pango la kinywa na ugeuzaji wa nafasi ya ulimi na muundo wa midomo. Kwa mintarafu hii, vokali huelezwa kuzingatia kwenda juu au kuwa chini kwa ulimi, nafasi ya ulimi kinywani na muundo wa mdomo.

### a) KWENDA JUU AU KUWA CHINI KWA ULIMI

Kigezo hiki huzingatiwa kwa mkumbo wa kwenda juu kutoka chini kwa ulimi kinywani. Kinachorejelewa hapa ni vile ulimi unavyokaribia paa la kinywa, kilele cha lamina. Ulimi huweza kuchukua nafasi tatu za kimsingi: juu au funge; kati au nusu funge/wazi; na chini au wazi.

#### i) Juu

Vokali ambayo ni ya juu huelezwa hivyo kwa sababu, katika kuitamka, ulimi huwa umefikia kilele chake. Vokali hiyo, pia, ni funge kwa sababu ulimi hukaribiana na paa la kinywa. Vokali hizi, katika Kinyala (K) ni /i/ na /u/ k.m.

/lira/ "lia" /uja/ "hama"

/tima/ "kimbia" /uka/ "ghuna au funika"

**ii) Kati**

Katika utoaji wa vokali ya kati, sehemu ya kilele ya ulimi huwa chini kidogo ikilinganishwa na utoaji wa /i/. Walakini, nafasi hii si ya chini na, hivyo ni ya kati. Vokali za Kinyala (K) ambazo ni za aina hii ni /e/ na /o/ k.m.

/sena/ "kanyaga" /ola/ "oza"

/seβ a/ "zaba" /ona/ "ona"

**iv) Chini**

Katika nafasi hii, ulimi huwa chini kabisa sakafuni mwa kinywa, na nafasi kati ya ulimi na paa la kinywa ni wazi kabisa. Vokali hizi katika Kinyala (K) ni /a/ k.m.


/alia/ "anakula"

/afwa/ "anakufa"


/aria/ "anaogopa"

Michoro ifuatayo inaonyesha vokali hizi zote.

Mchoro 3. Chati ya Vokali za Kinyala (K)




Mchoro 4. Mahali pa Kutamkia Vokali za Kinyala (K)




Vokali za Mbele

Vokali za Nyuma

b) **NAFASI YA ULIMI**

Kigezo hiki huzingatia kwenda upande - mbele au nyuma - ya kinywa. Hurejelea nafasi, kinywani, ambapo lamina ya ulimi huwapo.

Ulimi huweza kuwa katika sehemu ya mbele ya kinywa, sehemu ya katikati ya kinywa, na sehemu ya nyuma ya kinywa. Sehemu ya mbele huwa chini ya kaakaa ngumu ilhali ya nyuma huwa chini ya kaakaa laini. Ikiwa lamina i katikati ya kinywa, basi, huwa katika sehemu ya makutano ya kaakaa ngumu na kaakaa laini. Vokali za mbele katika Kinyala (K) ni kama vile:

/i/ katika /sima/ "zima"
/tʃina/ "choma"
/e/ katika /βetʃa/ "marafiki"
/jema/ "simama"

Vokali ya katikati ni /a/ kama vile katika /alia/ "anakula" au /asia/ "anasaga".

Kwa upande wake, vokali za nyuma ni:

/u/ katika /uja/ "hama"
/ula/ "tambua"
/o/ katika /ola/ "oza"
/osia/ "tongoza"

## a) MUUNDO WA MIDOMO

Muundo wa midomo hutoa kijelezi cha tatu cha kuelezea vipandesauti vya vokali. Katika hali hii, hali mbili za muundo wa midomo hutambuliwa: mviringo, ambao hutokea pale ambapo midomo huvutwa mbele; na bila mviringo, ambapo midomo huvutwa nyuma.

Vigezo hivi vitatu ndivyo vilivyotusaidia kueleza vokali za Kinyala (K). Kwa hivyo, katika kueleza vokali za Kinyala (K), ni muhimu kuwa tuanze na kwenda juu au kwenda chini kwa ulimi, ukifuatwa na nafasi ya ulimi na, hatimaye, muundo wa midomo. Hata hivyo, vigezo hivi, yafaa ieleweke, vina mipaka yake, kwani hutofautiana kutoka lugha moja hadi nyingine.

Kwa kuzingatia vigezo hivyo, hata hivyo, tunaweza kueleza vokali za Kinyala (K) ifuatavyo:

| Kwenda Juu au Chini kwa Ulimi | Nafasi ya Ulimi | Muundo wa Midomo |
|---|---|---|
| 1. /i/ juu/funge | mbele | si mviringo |
| 2. /e/ juu ya kati/nusu funge | mbele | si mviringo |
| 3. /a/ chini/wazi | katikati | si mviringo |
| 4. /o/ juu ya kati/nusu funge | nyuma | mviringo |
| 5. /u/ juu/funge | nyuma | mviringo |

Kutokana na deta hiyo, tunaona kuwa Kinyala (K) huwa na vokali tano (5). Licha ya hayo, kuna vokali ndefu katika lugha hii ambazo hupatikana pale ambapo vokali mbili sare zinafuatana bila

kudondosha moja. Hata hivyo, vokali hizi hazijitokezi, moja kwa moja, kama sauti bainifu k.m.

/u:/ katika luukha /lu:Xa/ "pumzika"
tuukha /tu:Xa/ "kuwa nyororo"
/o:/ katika soola /so:la/ "chomoa"
khoola /Xo:la/ "bandua"
/a:/ katika kaala /ka:la/ "pole pole"
saa /sa:/ "amrisha mbwa"

## 3.3 MFUATANO WA SAUTI ZA KINYALA (K)

Lugha hujengwa kwa ishara na sauti, lakini sauti zinazotumika ni zile za konsonanti na vokali. Lugha huundwa kwa sauti ndogo kabisa ziitwazo fonimu. Fonimu zikisimama pekee huwa hazina maana. Zinaungana kuunda silabi ambapo silabi huunda neno na maneno huunda vifungu ambavyo huunda sentensi.

### a) FONIMU KATIKA KINYALA

Fonetiki haijishughulishi na uchunguzi wa sauti za lugha maalum. Uchunguzi wa kifonetiki, wa lugha mahsusi, kwa hivyo, huishia katika uelezaji wa vipandesauti vya kifonetiki vipatikanavyo katika lugha husika. Vipandesauti hivi, vya kifonetiki, hujulikana kama foni. Chati ya Kimataifa ya Fonetiki ya Alfabeti - IPA - ni mfano mzuri wa chati ya foni. Vipandesauti vya kifonetiki hutofautishwa kwa kuwekwa katika mabano mraba [ ].

Fauka ya hayo, kuna njia badalia ya kufanyia uchunguzi wa sauti za lugha inayojulikana kama fonolojia. Fonolojia ni tawi la ismu

ambalo hujishughulisha na uchunguzi wa mifumo ya sauti za lugha mahsusi kama Kinyala (K). Katika mwanda huu, tunachunguza muundo wa sauti na utendakazi wake. Swali muhimu hapa ni: Je, sauti zitumiwazo kutofautisha maneno yenye maana tofauti zimechunguzwa? Katika Kinyala (K), kwa mfano, [p] na [k] huleta tofauti za maana katika maneno, kama vile ilivyo hapa chini:

/pala/ "doa"

/kala/ "zubaa"

/puka/ "funika kwa udongo"

/kuka/ "babu"

Katika fonolojia, vile vile, suala la sauti za lugha ambazo hazitofautishi maana ya maneno bali huonyesha njia badalia za utamkaji hujitokeza kama vile katika Kinyala (K):

/ŋgila/ au /ŋgira/ "njia"

Nia kuu ya sehemu hii ni kudhihirisha nafasi inayochukuliwa na fonimu katika hijai ya Kinyala (K), ikiwa na msingi wake katika herufi za alfabeti. Alfabeti ni kundi la alama zilizoandikwa na kuelezwa kama konsonanti na vokali, kila mojawapo ikiwakilisha aina moja ya sauti. Sauti hizi yafaa zitofautishe maana. Sauti au vipandesauti ambavyo husababisha tofauti ya maana katika maneno ya lugha mahsusi hujulikana, kiismu, kama fonimu (Anderson na Stageberg 1962:295). Fonimu huwekwa katikati ya mistari miwili / /. Inaweza kujadiliwa, kwa hivyo, kwamba dhana ya fonimu ndiyo chanzo cha maandishi ya kialfabeti. Katika alfabeti, kila fonimu

inawakilishwa na alama yake mahsusi na, hivyo, fonimu za vokali, kwa mfano, huwakilishwa na alama zinazojulikana, kiothografia, kama vokali. Kwa upande wake, fonimu za konsonanti huwakilishwa na konsonanti katika othografia. Katika kila lugha, kwa hivyo, alfabeti inayotumika katika othografia huzingatia ukubaliano au mshabaha kati ya alama moja na fonimu ambayo ambayo ni aina ya sauti moja. Katika Kinyala (K), kuna mshabaha mkubwa kati ya maandishi na mfumo wa utamkaji.

Tulitumia njia nne kuonyesha kwamba sauti za Kinyala (K) ni bainifu au si bainifu. Ubainifu, hapa, wamaanisha kwamba kuna mkinzano au tofauti. Licha ya kwamba tulitumia mbinu za kawaida za jozi mlinganuo finyu, kubadilishana umbo, na mgawo kamilishaji, tulipendekeza njia ya nne, ikiwa itakubaliwa, ya ulinganishi huru.

**i) Jozi Mlinganuo Finyu katika Kinyala**

Mbinu ya jozi mlinganuo finyu hutumiwa kuonyesha kwamba sauti mbili, katika lugha fulani, ni bainifu, na, hivyo, zinawakilisha fonimu tofauti. Ikiwa maneno mawili katika lugha fulani, yanatofautiana kimaana lakini hutofautiana, kifonolojia, kwa kipandesauti kimoja tu na vipandesauti vingine vikiwa na mpangilio sare, maneno hayo mawili huelezeka kama jozi mlinganuo finyu. Katika hali namna hii, sauti hizo, mbili, pale ambapo zinatofautiana, huchukuliwa kuwa ni fonimu mbili tofauti. Hii ni kwa sababu ubadilishaji wa moja na nyingine husababisha mabadiliko katika maana ya neno.

Ufuatao ni uchanganuzi wa fonimu za Kinyala (K) kuzingatia mbinu ya jozi mlinganuo finyu:

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 1. | pala /pala/ | "doa" | p \| á \| l \| á | = /p/ na /t/ |
| | tala /tala/ | "boma" | t \| á \| l \| á | |
| 2. | chema /tʃema/ | "kata" | tʃ \| é \| m \| á | = /tʃ/ na /t/ |
| | tema /tema/ | "jaribu" | t \| é \| m \| á | |
| 3. | suta /suta/ | "songa" | s \| ú \| t \| á | = /s/ na /k/ |
| | kuta /kuta/ | "gonga" | k \| ú \| t \| á | |
| 4. | pala /pala/ | "doa" | p \| á \| l \| á | = /p/ na /β/ |
| | bala /βala/ | "hesabu" | β \| á \| l \| á | |
| 5. | muna /muna/ | "sungura" | m \| ú \| n \| á | = /m/ na /n/ |
| | nuna /nuna/ | "nyonya" | n \| ú \| n \| á | |
| 6. | keka /keka/ | "beba" | k \| é \| k \| á | = /k/ na /tʃ/ |
| | cheka /tʃeka/ | "tega" | tʃ \| é \| k \| á | |
| 7. | numa /numa/ | "ninauma" | n \| ú \| m \| á | = /n/ na /ɲ/ |
| | nyuma /ɲuma/ | "nyuma" | ɲ \| ú \| m \| á | |
| 8. | ng'ala / ala/ | "kusudia" | ŋ \| á \| l \| á | = /ŋ/ na /j/ |
| | yala /jala/ | "tandika" | j \| á \| l \| á | |

9. khala /Xala/ "kaa" X | a | l | a

= /X/ na /h/

hala /hala/ "chapuka" h | a | l | a

10. wenya /wena/ "unataka" w | e | ɲ | a

= /w/ na /k/

kenya /kena/ "anataka" k | e | ɲ | a

11. lia /lia/ "kula" l | i | a

= /l/ na /r/

ria /ria/ "ogopa" r | i | a

12. firo /firo/ "mpingo" f | i | r | o

= /f/ na /v/

viro /viro/ "usiku wa siku nyingi" v | i | r | o

13. yema /jema/ "simama" j | e | m | a

= /e/ na /i/

yima /jima/ "nyima" j | i | m | a

14. sala /sala/ "sali" s | a | l | a

= /a/ na /o/

sola /sola/ "cheza" s | o | l | a

15. kula /kula/ "nunua" k | u | l | a

= /u/ na /o/

kola /kola/ "rudi" k | o | l | a

**ii) Ulinganishi Huru katika Kinyala**

Isipokuwa /f/ na /v/ ambazo zinaweza kuainishwa kwa msingi wa mkinzano wa uhafifu na ughunaji, aghalabu fonimu ghuna za Kinyala (K) zinaweza tu kuainishwa kwa kuzingatia mbinu tuliyopendekeza

ya ulinganishi huru. Katika ulinganishi huru, sauti za lugha zinaweza kupangwa kwa msingi wa jozi mlinganuo finyu. Walakini, katika ulinganishi huru, tunapata jozi mlinganuo finyu na sauti moja ikijitikeza huru bila kulinganishwa na nyingine, moja kwa moja.Ulinganishi huru hujitokeza pale ambapo fonimu ghuna hufuata nazali. Fonimu hizo ni /b/, /d/, /g/ na /ɟ/. Fonimu hizi zinaweza kulinganishwa kijozi ilhali zile nazali zinazohusiana nazo husimama pweke na vile vile hutambuliwa kama fonimu. Mifano inapatikana katika deta ifuatayo:

1. para /para/ "fikiri"

   mbara /mbara/ "ninafikiri"

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | p | a | r | a |
| ɱ | b | a | r | a |

= /p/, /ɱ/ na /b/

2. kola /kola/ "rudi"

   ngola / gola/ "ninarudi"

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | k | o | l | a |
| ŋ | g | o | l | a |

= /k/, /ŋ/ na /g/

3. tukha /tuXa/ "tusi"

   ndukha /nduXa/ "ninatusi"

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | t | u | X | a |
| n | d | u | X | a |

= /t/, /n/ na /d/

4. chula /tʃula/ "toka"

   njula /ɲJula/ "ninatoka"

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | tʃ | u | l | a |
| ɲ | ɟ | u | l | a |

= /tʃ/, /ɲ/ na /ɟ/

**iii) Kubadilishana Umbo katika Kinyala**

Kubadilishana umbo hutumiwa kudhihirisha kwamba tofauti au mkinzano, kati ya sauti mbili au zaidi za lugha, si bainifu na kwamba vipandesauti hivyo ni alofoni za fonimu moja.

Kubadilishana umbo hutokea pale ambapo mabadiliko, katika utamkaji wa neno fulani, hayasababishi mabadiliko kimaana ya neno husika. Katika hali hii, wazungumzaji wa lugha fulani hawasikii tofauti za kimatamshi au wanakubali utamkaji badalia kama sahihi. Zile sauti mbili ambazo huleta utamkaji badalia, kwa hivyo, huchukuliwa kama alofoni za fonimu moja.


Deta ifuatayo, kutoka Kinyala (K), ni dhihirisho la kubadilishana umbo:

/jitʃa/ ⟶ /jitsa/ "njoo"
/eloko/ ⟶ /eroko/ "urogi/uchawi"
/lalu/ ⟶ /ralu/ "ni kichaa"
/tʃia/ ⟶ /ria/ "ogopa"

Walakini, katika deta ifuatayo, sauti hizi zinatambuliwa kama fonimu tofauti kila moja:

yala /jala/ "tandika"
yara /jara/ "endesha"
loba /loβa/ "kataa"
roba /roβa/ "agua"
lia /lia/ "kula"
ria /ria/ "ogopa"
nyira /nira/ "tanua"
nyicha /nitʃa/ "kuwa baridi"
risia /risia/ "kemea"
chisia /tʃisia/"shinda"

Tunachosema hapa ni kwamba mzungumzaji anaweza kutumia /tʃ/ au /ts/ bila kubadilisha maana; /l/ na /r/ bila kubadilisha maana; na /tʃ/ au /r/ bila kubadilisha maana. Kinachojitokeza, hatimaye, ni:





**iv) Mgawo Kamilishaji Katika Kinyala**


Mgawo kamilishaji hutumiwa kuonyesha kuwa mkinzano au tofauti iliyopo kati ya sauti mbili si bainifu bali sauti husika ni alofoni za fonimu moja. Sauti mbili, katika lugha fulani, zinapopatikana katika mazingira tofauti ya kifonetiki, kiasi kwamba pale ambapo moja inatokea nyingine haipatikani, sauti hizo mbili husemekana kuwa katika mgawo kamilishaji. Sauti zipatikanazo katika mgawo kamilishaji huchukuliwa kuwa ni viwakilisho vya fonimu moja.

Sauti ambazo huwa katika mgawo kamilishaji huwa na sifa mbili kuu: huwa ni sare kifonetiki; na huwa na sababu ya kueleza tofauti zao za kifonetiki katika mazingira ya kifonetiki. Deta ya Kinyala ifuatayo itatoa ithibati:

| A | B |
|---|---|
| pala [pala] "ni doa" | mapala [mapala] "madoadoa" |
| pakha [paXa] "chachisha" | mapakhe [mapaXe] "yamechacha" |
| pukha [puXa] "kuwa chafu" | mupukhu [mupuXu] "mchafu" |
| tala [tala] "boma/mji" | matala [matala] "maboma/miji" |
| tema [tema] "jaribu" | matemo [matemo] "majaribu" |
| takha [taXa] "tafuta" | matakho [mataXo] "matako" |

Ukichukua karatasi na uiweke mbele ya mdomo, wakati wa kutamka maneno katika kundi (A), utagundua kwamba yana mpumuo zaidi ya yale ya kundi (B). Kwa kutilia makini matamshi ya [p] na [t], katika maneno hayo, itagunduliwa kwamba [p] na [t], katika maneno ya kundi (A) zinatamkwa tofauti na [p] na [t] za kundi (B). Sababu ya tukio hili ni kwamba [p] na [t], katika kundi (A) zinatamkika kwa nyongeza fulani ya pumzi, ambayo inaitwa mpumuo. Jambo la kuzingatia hapa ni kwamba [$p^h$] na [$t^h$] (zilizo na mpumuo), aghalabu, hutokea katika mazingira ya mwanzo, ilhali zile zisizo na mpumuo hutokea mahali pengine pale. Katika hali namna hii, tunaweza kusema kuwa [$p^h$] na [$t^h$] ni alofoni za fonimu /p/ na /t/. Yaani:




[$p^h$] na [$t^h$] zenye mpumuo, pia, zimo katika mgawo kamilifu kwa sababu mazingira zinamotokea ni tofauti: [$p^h$] na [$t^h$] hupatikana katika mazingira awali ya neno; na [p] na [t] hutokea katika mazingira kativokali.

**b) SILABI KATIKA KINYALA**

Maneno na sehemu kubwa za uneni hutiliwa mipaka ya silabi kuzingatia mfumo wa mpangilio wa silabi katika lugha husika. Silabi, kwa hivyo, ni tamko la kimsingi kabisa katika neno, yaani ni sauti ambayo inatangulia kituo katika matamshi. Kwa mintarafu hii, tutaieleza silabi kama tamko kamili katika neno, ambalo laweza kuwa ni vokali tu, konsonanti na vokali au konsonanti zaidi ya moja na vokali.

**a) Silabi ya Vokali Tu**

Silabi ya vokali tu, katika Kinyala, hutokea kama mwandamano wa vokali mbili bila konsonanti. Deta ifuatayo ni dhihirisho la silabi ya aina hiyo:

| | | | |
|---|---|---|---|
| ao | a$o | "hapo" | V$V |
| oa | o$a | "funga" | V$V |
| ou | o$u | "huo" | V$V |
| oe | o$e | "fungeni" | V$V |
| aa | a$a | "hapa" | V$V |

**b) Silabi ya Konsonanti na Vokali**

Aina hii ya silabi hutokea pale ambapo konsonanti moja hufuatwa na vokali, na kuzua mwandamano KV. Mdokezo huu unaweza kufafanuliwa na deta ifuatayo:

| | | | |
|---|---|---|---|
| fula | fu$la | "vuja au mvua" | KV$KV |
| tira | ti$ra | "shika" | KV$KV |
| suma | su$ma | "omba kwa jamaa" | KV$KV |
| sulula | su$lu$la | "vuja" | KV$KV$KV |
| loma | lo$ma | "sema" | KV$KV |
| kuma | ku$ma | "meza mrututu" | KV$KV |

**c) Silabi ya Konsonanti Zaidi ya Moja na Vokali**

Silabi hii hutokea pale ambapo kuna mwandamano wa konsonanti zaidi ya moja zikifuatwa na vokali. Kwanza, kunawea kuwa na mfuatano wa konsonanti mbili na vokali, pale ambapo tuahusisha baadhi ya nasali na sauti nyingine za mguno, ambapo katika lugha hii, sauti ghuna /b, d, g, ɟ/ haziwezi kutokea mwanzoni mwa neno au silabi:

| | | | |
|---|---|---|---|
| mbola | mbo$la | "ninasema" | KKV$KV |
| mbuka | mbu$ka | "ninamaka" | KKV$KV |

| | | | |
|---|---|---|---|
| ngola | ngo$la | "ninarudi" | KKV$KV |
| ngala | nga$la | "sarafu au ninazubaa" | KKV$KV |
| ndulu | ndu$lu | "ni kali" | KKV$KV |
| ndekhe | nde$Xe | "niwache/imepikwa" | KKV$KV |
| njala | nja$la | "njaa" | KKV$KV |
| njekha | nje$Xa | "ninacheka" | KKV$KV |

Pia, tunaweza kuwa na mfuatano wa nasali na nusu vokali, kama ifuatavyo:

| | | | |
|---|---|---|---|
| lumwa | lu$mwa | "umwa" | KV$KKV |
| munwa | mu$nwa | "mdomo" | KV$KKV |
| nywa | nywa$ | "kunywa" | KKV$ |

Isitoshe, nusu vokali /j/ na /w/ huweza kufuatana, hususan, /j/ hutangulia na kufuatwa na /w/, kama vile katika:

| | | | |
|---|---|---|---|
| khaywa | Xa$jwa | "kosa" | KV$KKV |
| oweywe | o$we$jwe | "aina ya nyasi" | V$KV$KKV |
| seywa | se$jwa | "tusiwa" | KV$KKV |

Wakati mwingine, vituo /p, t, k/, vikwaruzo /f, s/, kikwamiza /β/ na kitambaza /l/ huja kabla ya /w/ k.m.

| | | | |
|---|---|---|---|
| khupwa | Xu$pwa | "pigwa" | KV$KKV |
| tupwa | tu$pwa | "tupwa" | KV$KKV |
| sotwa | so$twa | "tiwa" | KV$KKV |
| futwa | fu$twa | "futwa" | KV$KKV |

| | | | |
|---|---|---|---|
| kwa | kwa$ | "anguka" | KKV$ |
| chukwa | tʃu$kwa | "tawaliwa" | KV$KKV |
| fwa | fwa$ | "kufa" | KKV$ |
| fwala | fwa$la | "vaa" | KKV$KV |
| swekha | swe$Xa | "toroka" | KKV$KV |
| swaka | swa$ka | "swaga" | KKV$KV |
| sabwa | sa$ wa | "ombwa" | KV$KKV |
| ibwa | i$ wa | "ibwa" | V$KKV |
| lwala | lwa$la | "kidole au ugua" | KKV$KV |
| lweyo | lwe$jo | "ufagio" | KKV$KV |

Kuna pia mfuatano changamano wa sauti unaohusisha nazali, vituo ghuna na nusu vokali, hususan, /w/ ambapo konsonanti tatu huweza kufuatana na kuunda silabi moja tu pamoja na vokali:

| | | | |
|---|---|---|---|
| ndwala | ndwa$la | "ninaugua" | KKKV$KV |
| ndwolwo | ndwo$lwo | "ndiyo hiyo" | KKKV$KKV |
| ngwekho | ŋgwe$xo | "niangukie" | KKKV$KV |
| ngwoyo | ŋgwo$jo | "ndiye huyo" | KKKV$KV |
| ngwono | ŋgwono | "ndiye huyu" | KKKV$KV |
| mbwekho | mbwe$xo | "wachana na mimi" | KKKV$KV |
| mbwa | mbwa$ | "mbwa" | KKKV$ |
| mbwao | mbwa$o | "ninaenda nyumbani" | KKKV$V |
| mbwana | mbwa$na | "ninawasha" | KKKV$KV |

### c) MOFIMU KATIKA KINYALA

Neno mofimu linatokana na tawi la ismu lijulikanalo kama mofolojia. Mofolojia ni tawi la ismu linalojishughulisha na

muundo wa ndani wa maneno (Bloomfield 1933 na Mathews 1974). Kipashio cha kimsingi sana kinachozingatiwa na wanamofolojia ni kile kinachojulikana kama mofimu.

Mofimu ni kipashio kidogo zaidi cha kisarufi chenye maana. Bloomfield (1933) anasema kuwa kipashio hiki ndicho kidogo kuliko vyote kwa sababu hakiwezi kugawika zaidi pasipo kupoteza maana ya umbo hilo. Mofimu Kinyala (K) hujitokeza kama: neno kamili yaani neno lisilogawika kama vile mbwa (mbwa), nyuni (ndege), nyanga (jua), mwesi (mwezi) n.k.; mzizi wa neno k.m. -ana (toto), -sacha (ume) n.k. baada ya kuondoa viambishi mw- na mu-; na kiambishi k.m. nafsi katika n-dia, a-lia, o-lia (kula) - kwanza, pili na tatu yaani ninakula, anakula na unakula.

Mathews (1974) anazungumzia juu ya aina mbili za mofimu ziwezazo kugawika kama mofimu za kileksia yaani mofimu zinazotambulisha leksimu au neno lenyewe kama vile ng'ombe, mbusi (mbuzi), kondi (kondoo) n.k. na zile ambazo ni mofimu ambishaji k.m. -som- tunaweza kuambisha na kupata asoma (anasoma), asomesa (anasomesha), musomi (mwanafunzi), ambapo tuanpata kuwa soma ni mofimu ya kileksia ambayo tumeiongezea viambishi na kupata yale maneno mengine.

Mofimu katika Kinyala (K) hujitokeza pia kama huru, tegemezi na kapa. Mofimu huru hujisimamia bila kutegemea nyingine kwa kukamilisha maana. Mofimu huru katika Kinyala (K) ni kama vile:

| | |
|---|---|
| mama | "mama" |
| papa | "baba" |
| lulu | "kali" |
| nulu | "tamu" |
| mali | "nyeusi" |

Mofimu tegemezi haziwezi kuleta maana kivyake maadam ni funge na hutegemea mofimu nyingine yaani lazima ziambatanishwe na mofimu nyingine. Mofimu hizi katika Kinyala (K) hujitokeza kama viini vya vitenzi kama vile tulivyoeleza katika mfano wa -som-. Mofimu kapa (mofimu ∅), kwa upande wake, ni umbo linalopungua katika uwasilishi wake kifonolojia ijapokuwa maana ipo. Mofimu za aina hii, katika Kinyala (K) hudhihirika katika baadhi ya majina katika hali ya kuonyesha wingi, hususan, yale ambayo hayabadiliki, kama vile mbusi (mbuzi), swa (kumbikumbi), mbwa (mbwa), ngokho (kuku), ng'ombe (ng'ombe) n.k.

Wasemavyo wanamofolojia, mofimu ni dhana ya kidhahania ambayo imezua migogoro mingi. Baadhi ya masuala yanayohusiana na migogoro hii ni: Je, mofimu kapa ni mofimu bila mofu? Je, kuna uwezekano wa mofimu kapa kuwa na alomofu/vibadala? Je, dhana ya kapa ina maana yoyote? Maswali kama haya, yafaa izingatiwe, yako nje ya kazi yetu. Tunachopaswa kuelewa kwa hivi sasa ni kwamba mofimu kapa haitambulishwi. Aghalabu, mofimu hufanana na silabi, na mfanano huu ni wa kisadifa tu kwa sababu silabi haina maana.

Dhana ambayo tumeirejelea hapo juu ya mofu ni vipande vya neno ambavyo vimesetiri mofimu (hubeba mofimu). Mara nyingi, mofu ni

utambulishi wa kipashio cha kifonolojia kinachowakilisha mofimu. Kila mofu huwasilisha maana fulani. Jambo la kuzingatia ni kwamba si lazima idadi ya mofu iende sambamba na idadi ya mofimu ndiposa, kutokana na mifano tuliyotoa, tuliona kwamba mofimu kapa haina mofu tuwezazo kutambulisha.

Dhana nyingine muhimu ni alomofu, ambayo ni maumbo mbalimbali (vibadala vya) ya mofimu moja. Alomofu katika Kinyala (K) ni kama vile <u>si</u>achia, <u>su</u>chia (haendi, huendi) yaani "si" na "su" ni mofimu moja kanushi, ambapo "si" hurejelea nafsi za kwanza na tatu ilhali "su" hurejelea nafsi ya pili.

**4.4 HITIMISHO**

Katika sura hii, maelezo yametolewa jinsi sauti za Kinyala (K) zinavyotolewa na jinsi ya kuweza kuziainisha. Maelezo yametolewa pia jinsi ya kuweza kutambua fonimu katika Kinyala (K) ambapo fonimu ishirini na saba (27) zimetambuliwa: konsonanti isirini na mbili na vokali tano. Katika maelezo hayo, mbinu iliyozingatiwa sana ni ya jozi mlinganuo finyu na pale ambapo mbinu hii haingeweza kueleza baadhi ya fonimu, mbinu iliyopendekezwa ya ulinganishi huru ilitumiwa. Pia alofoni za Kinyala (K) zilitambuliwa kwa kutumia mbinu za kubadilishana umbo na mgawo kamilishaji. Pia silabi katika Kinyala (K) zilibainishwa ambazo ni za aina tatu: silabi ya vokali tu, silabi ya konsonanti na vokali na silabi ya konsonanti zaidi ya moja na vokali. Isitoshe, mofimu, mofu na alomofu za lugha hii zilielezwa.

## SURA YA NNE

## MIFANYIKO YA KIFONOLOJIA KATIKA KINYALA (K)

### 4.0 UTANGULIZI

Dhana ya kanuni asilia ni zao la juhudi za kutaka kueleza, kindakindaki na wazi, mifanyiko ya kifonolojia inayotokea katika lugha. Mofimu zinapounganishwa kuunda maneno, vitamkwa vya mofimu jirani huathiriana na, wakati mwingine, hubadilika. Hivi ndivyo inavyotukia, kwa mfano, katika maneno ya Kiingereza <u>electric</u>, <u>electrical</u>, <u>electricity</u> na <u>fanatic</u>, <u>fanatical</u> na <u>fanaticism</u>, ambapo /k/ ya mwisho katika <u>electric</u> na <u>fanatic</u> inageuka na kuwa /s/ kabla ya mofimu inayoanza na /i/. Mabadiliko, pia, hutokea katika mazingira ambayo si lazima mofimu mbili zije pamoja. Hili, kwa mfano, laweza kutokea mwanzoni au mwishoni mwa neno au katika hali ambapo nafasi ya kitamkwa inaweza kuzingatiwa sambamba na vokali yenye mkazo. Mabadiliko haya ndiyo yanayojulikana kama mifanyiko ya kifonolojia.

Katika sura hii, mifanyiko ya kifonolojia katika Kinyala (K) itaelezwa kwa kuichambua deta iliyopatikana nyanjani. Deta hii ilipatikana kwa njia ya uchunguzi-shiriki katika mazungumzo ya kawaida na kurekodiwa kwenye kanda na kunakiliwa. Pia ujuzi wa watafiti kama waongeaji asilia wa Kinyala ulichangia pakubwa.

### 4.1 WIANO KATIKA KINYALA

Katika mazungumzo ya kawaida, tunapozungumza, baadhi ya maneno hutamkika mbalimbali. Walakini, katika uzungumzi unaoendelea,

vitamkwa fulani, vinavyotokana na neno, huweza kusababisha mabadiliko katika neno jingine, hususan, neno jirani. Fonimu ya neno moja inapoathiri matamshi ya neno jingine huitwa wiano. Wiano, pia, huhusisha hali ambapo kitamkwa huathiri kitamkwa jirani.

Kwa hivyo, katika mfanyiko wa wiano, kitamkwa huchukua sifa kutoka kwa kitamkwa jirani. Jambo hili hutokea katika hali mbili, ambazo ni wiano mbele na wiano nyuma. Kwa mfano, konsonanti huweza kuchukua sifa za vokali, vokali ichukue sifa za konsonanti, konsonanti moja inaweza kuathiri nyingine au vokali iiathiri nyingine. Hali hii huhusisha unasalishaji, ughunaji, wiano pamwe wa nazali (homorganic nasal assimilation), ukaakaishaji na tangamano vokali. Asemavyo Schane (1972), wiano ni mfano mzuri sana wa kaida ambazo zina sifa fulani jumuishi (ndipo zikaitwa sifa za wiano); vitamkwa fulani hubadilika ili kukubaliana na sifa fulani za vitamkwa jirani. Mifano ifuatayo itafafanua dhana hii.

**a) Konsonanti Huwiana na Sifa za Vokali**

Mifanyiko ya aina hii hutokea sana katika ukaakaishaji. Nafasi inayochukuliwa na ulimi wakati wa kutamka vokali ya mbele hulazimishwa kwa konsonanti jirani. Vokali mbili huweza kuungana na kuwa nusu vokali na, hatimaye, vokali:

2V $\longrightarrow$ nusu vokali

/siuma/ $\longrightarrow$ [sjuma] "ushanga"

/siula/ ⟶ [sjula] "ng'oa"

/siema/ ⟶ [sjema] "kinasimama"

/sioki/ ⟶ [sjoki] "kali"

/siaka/ ⟶ [sjaka] "kinapalilia"

Katika deta hiyo, tunaona kuwa vokali /i/ inapokurubiana na vokali nyingineyo, inabadilika na kuwa kiyeyusho /j/. Mabadiliko haya yanajulikana kama uuundaji wa viyeyusho au uyeyushaji. Kanuni hapa ni kwamba:

i ⟶ j/___ [+ vokali]

Wakati mwingine, kuna mabadiliko ya vokali iliyotumiwa k.m.

/muana/ ⟶ [mwana] " mtoto"

/muera/ ⟶ [mwera] "mabaki ya nafaka"

/muiβi/ ⟶ [mwiβi] "mwizi"

/luala/ ⟶ [lwala] "ugua"

/nduala/ ⟶ [ndwala] "ninaugua"

/luejo/ ⟶ [lwejo] "ufagio"

/luana/ ⟶ [lwana] "pambana au utoto"

/sueXa/ ⟶ [sweXa] "toroka"

/omuiXo/ ⟶ [omwiXo] "jamaa au mwiko"

Katika deta hii, tunaona kuwa vokali /u/ inabadilika na kuwa nusu vokali /w/, ambapo kanuni inakuwa:

u ⟶ w/___ [+ vokali]

Kuhusu uviringishaji, nafasi inayochukuliwa na ncha ya ulimi katika kutamka vokali mviringo inasababisha kuweko kwa konsonanti. Katika hali hii, konsonanti hukaakaishwa zinapotokea kabla ya vokali za mbele na kuviringishwa kabla ya vokali mviringo, kama vile ilivyo hapa chini:

Ukaakaishaji

k$^y$iene /kiene/ ⟶ [kjene] "wenyewe (hali ya ukubwa)"

k$^y$ikie /kik$^y$ie/ ⟶ [kjikje] "yake (hali ya ukubwa)"

ch$^y$iene /tʃiene/ ⟶ [tʃjene] "zenyewe"

Uviringishaji

k$^w$ul$^w$u /kulu/ ⟶ [kwulwu] "mbingu"

k$^w$uk$^w$u /kuku/ ⟶ [kwuku] "ufuo"

och$^w$unj$^w$u /o unju/ ⟶ [otʃwunjwu] "vitu (hali ya udogo)"

Kanuni hapa, kwa ukaakaishaji, ni kuwa:

$$\begin{bmatrix} -\text{ Konsonanti} \\ \\ -\text{ Kaakaa} \end{bmatrix} \longrightarrow \begin{bmatrix} +\text{ Konsonanti} \\ \\ +\text{ Kaakaa} \end{bmatrix} \Big/ \begin{bmatrix} +\text{ Vokali} \\ \\ +\text{ Mbele} \end{bmatrix}$$

Kwa upande wa uviringishaji, tunapata kuwa:

$$\begin{bmatrix} -\text{ Konsonanti} \\ \\ -\text{ Mviringo} \end{bmatrix} \longrightarrow \begin{bmatrix} +\text{ Konsonanti} \\ \\ +\text{ Mviringo} \end{bmatrix} \Big/ \begin{bmatrix} +\text{ Vokali} \\ \\ +\text{ Nyuma} \end{bmatrix}$$

**b) Vokali Huwiana na Sifa za Konsonanti**

Kanuni hii husema kuwa sifa za konsonanti huweza zikalazimishwa juu ya vokali. Mabadiliko yanayotokea, katika aina hii ya wiano, ni ya kialofoni. La kukumbukwa ni kuwa, aghalabu, vokali hunazalishwa kifonetiki zikikurubiana na konsonanti ya kinazali. Mfanyiko huu unajitokeza katika deta ifuatayo:

| | | |
|---|---|---|
| nyuma | [ɲũma] | "nyuma" |
| nyuni | [ɲũni] | "nyuni/ndege" |
| ng'ina | [ŋĩna] | "mamake au ninametameta" |
| ng'oni | [ŋõni] | "mwendo wa pole" |
| ng'ombe | [ŋõmbe] | "ng'ombe" |
| nuni | [nũni] | "ufuta" |
| muma | [mũma] | "sina au vibonge" |

Kanuni hapa ni kwamba:

$$\underset{[-\text{ Nasali}]}{V} \longrightarrow \underset{[+\text{ Nasali}]}{V} / ___ \underset{[+\text{ Nasali}]}{K}$$

**c) Konsonanti Huwiana na Sifa za Konsonanti**

Jambo litukialo, sana sana, ni kwa mlolongo wa konsonanti kukubaliana kwa kauli au ughunaji. Kwa mfano, konsonanti ya kinasali huwa pamwe na konsonanti inayoifuata, ambapo tunaona kuwa sauti ya mtuo /p/ inabadilika na kuwa /b/, katika mfano ufuatao:

(lu)pau [lupau] "ubao"

| | | |
|---|---|---|
| mbau | [ɱbau] | "mbao" |
| para | [para] | "fikiri" |
| mbara | [ɱbara] | "ninafikiri" |

Tunaona, pia, katika mifano:

| | | |
|---|---|---|
| kova | [kova] | "sindikiza" |
| ngova | [ŋ gova] | "ninasindikiza" |
| kama | [kama] | "tia tembo maji" |
| ngama | [ŋ gama] | "ninatia tembo maji" |
| kiva | [kiva] | "gonga" |
| ngiva | [ŋ giva] | "ninagonga" |
| kuma | [kuma] | "jikaze au jikakamue" |
| nguma | [ŋ guma] | "ninajikakamua" |
| kava | [kava] | "gawa" |
| ngava | [ŋ gava] | "ninagawa" |
| kula | [kula] | "nunua" |
| ngula | [ŋ gula] | "ninanunua" |

Katika deta hiyo, /k/inabadilika na kuwa /g/ baada ya konsonanti ya kinasali. Mfano mwingine unahusu /t/ ambayo inabadilika na kuwa /d/ katika:

| | | |
|---|---|---|
| tala | [tala] | "weka dhamana" |
| ndala | [ndala] | "ninaweka dhamana" |
| tula | [tula] | "laumu" |
| ndula | [ndula] | "ninalaumu" |
| tira | [tira] | "shika" |

| | | |
|---|---|---|
| ndira | [ndira] | "ninashika" |
| tamba | [tamba] | "kuwa fukara" |
| ndamba | [ndamba] | "nimekuwa fukara" |
| tima | [tima] | "kimbia au potea njia" |
| ndima | [ndima] | "ninakimbia au nimepotea njia" |
| tukha | [tuXa] | "tusi" |
| nduhka | [nduXa] | "ninatusi" |
| tema | [tema] | "jaribu" |
| ndema | [ndema] | "ninajaribu" |

Kanuni hapa, kwa jumla, ni kwamba:

$$\begin{bmatrix} +\text{ Mtuo} \\ -\text{ Ghuna} \end{bmatrix} \longrightarrow [+\text{ Ghuna}] / [+\text{ Nasali}]___$$

Hali kadhalika, /tʃ/ hubadilika na kuwa /ɟ/ baada ya nasali:

| | | |
|---|---|---|
| chala | [tʃala] | "toa damu kwa ng'ombe" |
| njala | [ɲɟala] | "ninatoa damu kwa ng'ombe" |
| chuka | [tʃuka] | "tawala/kuwa majimaji" |
| njuka | [ɲɟuka] | "ninatawala/ni majimaji" |
| chukha | [tʃuXa] | "mwaga" |
| njukha | [ɲɟuXa] | "ninamwaga" |

Kanuni hapa ni kuwa:

$$\text{tʃ} \longrightarrow \text{ɟ}/\text{N}___$$

Isitoshe, katika lugha hii (Kinyala K), /l/ hubadilika na kuwa /d/ na /ɟ/ na /j/ hubadilika na kuwa /ɟ/ katika hali ya nasali kuwa pamwe na konsonanti inayokurubiana nayo:

| | | |
|---|---|---|
| lecha | [letʃa] | "leta" |
| ndecha | [ndetʃa] | "ninaleta" |
| lela | [lela] | "lea" |
| ndela | [ndela] | "ninalea" |
| lusa | [lusa] | "tapika" |
| ndusa | [ndusa] | "ninatapika" |
| leka | [leka] | "dharau" |
| ndeka | [ndeka] | "ninadharau" |
| lekha | [leXa] | "wacha" |
| ndekha | [ndeXa] | "ninawacha" |
| lwika | [lwika] | "pembe (umoja)" |
| njika | [ɲɟika] | "pembe (wingi)" |

Katika deta hiyo, tunaona kuwa:

l ⟶ { d, ɟ } /N___

Katika deta:


| | | |
|---|---|---|
| yuka | [juka] | "tembea kwa kasi" |
| njuka | [ɲɟuka] | "ninatembea kwa kasi" |
| yula | [jula] | "chukua upesi" |
| njula | [ɲɟula] | "ninachukua upesi" |

j ⟶ ɟ/N___

Kanuni jumuishi hapa ni:

$$\begin{bmatrix} +\text{Konsonanti} \\ -\text{Ghuna} \end{bmatrix} \longrightarrow \begin{bmatrix} +\text{Konsonanti} \\ +\text{Ghuna} \end{bmatrix} / \begin{bmatrix} +\text{Konsonanti} \\ +\text{Nazali} \end{bmatrix} __$$

Katika deta tuliyorejelea, [N] ilichukuliwa kusimamia nazali kama vile ilivyo hapa chini:




Katika hali namna hiyo, inapatikana, pia, kwamba /n/ huweza kubadilika na kuwa /ɲ/ au /ŋ/ na /m/ ikabadilika na kuwa /ɱ/ kama vile katika:

| | | |
|---|---|---|
| njala | [ɲɟala] | "njaa au ninatoa damu kwa ng'ombe" |
| njukha | [ɲɟuXa] | "ninamwaga" |
| njuka | [ɲɟuka] | "ninatawala au ni majimaji" |
| njava | [ɲɟava] | "ninachimba" |

n __________ ɲ/___ ɟ

Katika:

| | | |
|---|---|---|
| ngona | [ŋ gona] | "ninalala" |

| | | |
|---|---|---|
| ngila | [ŋgila] | "njia" |
| nguyu | [ŋguju] | "huyu" |
| ngaye | [ŋgaje] | "nikataze" |
| nganya | [ŋgana] | "ninakubali" |
| ngula | [ŋgula] | "ninanunua" |
| ngofu | [ŋgofu] | "kuukuu" |
| ngutu | [ŋgutu] | "fupi" |
| ngokho | [ŋgoXo] | "kuku" |
| ngiri | [ŋgiri] | "ngiri" |
| nguke | [ŋguke] | "nyani" |

n ———————— ŋ /___ g

Katika:

| | | |
|---|---|---|
| mbara | [ɱbara] | "ninafikiri" |
| mbau | [ɱbau] | "mbao" |
| mbuka | [ɱbuka] | "ninamaka" |
| mbukha | [ɱbuXa] | "ninachafuka" |

m ————→ ɱ/___ b

**d) Vokali Huwiana na Sifa za Vokali (Tangamano Vokali)**

Katika mfanyiko huu, vokali ya silabi moja huweza kuwa kama sawa na vokali ya silabi nyingine. Hii ndiyo ijulikanayo kama tangamano vokali, ambayo yamaanisha kuwa vokali zote katika kikundi maalum hukubaliana katika sifa fulani za kifonetiki. Walakini, wanaismu wamekumbwa na tatizo la kuainisha tangamano vokali kama sifa ya vitamkwa au vikundi vya kisarufi, ambavyo ni

vikubwa kuliko vitamkwa, kama vile, kwa mfano, mashina ya maneno. Hizi ni aina mbili za tangamano vokali kama vile itakavyojitokeza katika makala haya.

Mwanaismu, Aoiki (Abercrombie, 1965 na 1967), amejaribu kutoa vigezo vya kuainisha mifumo ya tangamano vokali kamili na ile isiyo kamili. Katika tangamano vokali kamili, ambayo pia inaweza kuonekana kama uradidi, vokali ya mofimu huchukua sifa za vokali nyingine kabisa. Katika Kinyala (K), vitenzi:

| | | |
|---|---|---|
| mbe | /mbe/ | "nipe" |
| ndeche | /ndetʃe/ | "nilete" |
| khese | /Xese/ | "nisalimu" |

huchukua, kuonyesha kauli ya kutendewa, konsonanti ya kimadede /r/ ikifuatwa na mwigo wa vokali ya kitenzi-shina kuzua:

| | | |
|---|---|---|
| mbere | /mbere/ | "mpe kwa niaba yangu" |
| ndechere | /ndetʃere/ | "niletee kwa niaba yangu" |
| khesere | /Xesere/ | "msalimu kwa niaba yangu" |

Pia, tuanaweza kupata:

| | | |
|---|---|---|
| mbe | /mbe/ | "nipe" |
| mbese | /mbese/ | "nipe mimi" |

Yaani, konsonanti ya kikwaruzo /s/ inafuatwa na mwigo wa vokali ya kitenzi shina.

## 4.2 MIFANYIKO YA MIUNDO YA SILABI KATIKA KINYALA

Mifanyiko ya miundo ya silabi huathiri uenezaji wa konsonanti na vokali katika neno. Michakato hii huhusisha udondoshaji au uchopekaji wa konsonanti na vokali. Wakati mwingine, vitamkwa viwili vinaweza kuungana na kuzua kitamkwa kimoja. Katika hali nyingine, kitamkwa kinaweza kubadilisha sifa kuu za aina yake, jambo ambalo litamaanisha, kwa mfano, kuwa vokali inakuwa kiyeyusho. Kisha, vitamkwa viwili huweza kusababisha mabadiliko katika muundo asilia wa silabi.

Katika fonolojia, inasemekana kuwa silabi yenye muundo KV, unaohusiana na silabi iliyo na konsonati moja na vokali ndio muundo wa kimsingi kabisa. Isitoshe, mfanyiko wowote, ambao hupunguza muundo wa silabi changamano na kuzua ruwaza ya KV, huelekeza kwa kile kinachoitwa muundo wa silabi unaopendelewa zaidi. Lengo kuu la mfanyiko huu ni kuvunja mlolongo wa konsonanti au mwandamano wa vokali. Kwa mfano, mlolongo wa konsonanti mbili unaweza kurahisishwa kwa kudondosha mojawapo ya konsonanti hizo; kuchopeka vokali kati ya konsonanti hizo; na kuunganisha konsonanti hizo na kuwa kitamkwa kimoja.

**a) Kudondoshwa kwa Konsonanti**

Silabi ya Kinyala (K), aghalabu, huwa na muundo unaopendelewa zaidi wa KV. Hata hivyo, wakati ambapo kunatokea mfuatano wa KK, konsonanti moja hudondoshwa. Hili hutokea sana pale ambapo kuna konsonanti ya nazali inayofuatana na konsonanti ya kituo. Tunaona konsonanti /b/ ikidondoshwa inapopatikana karibu na nazali /m/ kabla ya vokali ya nyuma katika:

| | | |
|---|---|---|
| mbona | [mbona] | "ninaona" |
| mona | [mona] | "ninaona" |
| mbuma | [mbuma] | "sina" |
| muma | [muma] | "sina" |

Tunaona, katika mfano huo kuwa:

$$b \longrightarrow \emptyset / __ \begin{bmatrix} + \text{Vokali} \\ \\ + \text{Nyuma} \end{bmatrix}$$

Matokeo ni kwamba tunapata muundo wa silabi unaopendelewa zaidi wa KV ingawa maana ya neno haibadiliki.

**b) Kudondoshwa kwa Vokali**

Katika Kinyala (K), vokali hudondoshwa ikiwa neno linalofuata huanza kwa vokali. Udondoshaji huu huzuia vokali mbili kuja pamoja k.m.

| | | |
|---|---|---|
| chula eyo | /tʃula ejo/ | "toka huko" |
| chulayo | /tʃulajo/ | "toka huko" |
| khesa eyo | /Xesa ejo/ | "salimia huko" |
| khesayo | /Xesajo/ | "salimia huko" |
| khasira eyo | /Xasira ejo/ | "katalia huko" |
| khasirayo | /Xasirajo/ | "katalia huko" |

Tunachoona hapa ni kwamba vokali /e/ inadondoshwa ili kuondoa utata ambao ungetokea, kimatamshi, katika kuunganisha vokali [a] na [e]. Udondoshi huo, yafaa izingatiwe, hausababishi tofauti kimaana.

Mifano mingine ni kama vile:

ba + ana ⟶ bana [βana] "watoto"

ba + afurika ⟶ bafurika [βafurika] "Wafrika"

**c) Uchopekaji wa Konsonanti**

Uchopekaji wa konsonanti hutokea katika Kinyala (K), ambapo konsonanti [tʃ] huchopekwa ili kuvunja mlolongo wa vokali bila kubadilisha maana, kama vile ilivyo katika:

| | | |
|---|---|---|
| lianga | [liaŋga] | "uwe ukila" |
| lichanga | [litʃaŋga] | "uwe ukila" |
| chianga | [tʃiŋga] | "uwe ukienda" |
| chichanga | [tʃitʃaŋga] | "uwe ukienda" |

**d) Uchopekaji wa Vokali**

Katika Kinyala (K), ni mazoea kwamba maneno hayaishii kwa konsonanti. Katika hali namna hii, vokali huchopekwa ili kuendeleza mtindo wa silabi ya Kinyala wa KV. Aghalabu, maneno yanayochopekwa vokali ni ya mkopo. Deta ifuatayo ni dhihirisho la madai hayo:

Mwafrika (Kiswahili) ⟶ Mwafurika

Maalum (Kiswahili) ⟶ maalumu

labda (Kiswahili) ⟶ laputa

rocket (Kiingereza) ⟶ roketi

socket (Kiingereza) ⟶ soketi

bag (Kiingereza) ⟶ paka

### e) Muungano wa Konsonanti

Konsonanti mbili sanjari hubadilishwa na moja tu, ambayo ina sifa sawa na zile mbili asilia. Muungano, tunaweza kudai, huhusisha hali fulani ya wiano. Katika Kinyala (K), vitamkwa viwili vya kinazali [n] na [g] vinapotokea kisanjari, wakati mwingine, hubadilishwa na kitamkwa kimoja tu cha king'ong'o [ ] k.m.

| | | |
|---|---|---|
| nga'ng'a | [ŋaŋa] | "dinda" |
| ng'ala | [ŋ ala] | "kusudia" |
| khong'a | [Xoŋ a] | "gonga" |
| ng'asa | [ŋ asa] | "enea" |

### f) Muungano wa Vokali

Vokali mbili huungana ili kupunguza mlolongo wa vokali na kuzua muundo wa silabi ambao ni rahisi kama vile inavyodhihirika katika deta ifuatayo:

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| a + i | → | e k.m. ma + ino | → | meno | "meno" |
| a + o | → | o k.m. ma + oni | → | moni | "macho" |
| a + i | → | a k.m. ma + ingi | → | mangi | "mengi" |

## 4.3 KUDHOOFIKA NA KUPATA NGUVU KATIKA KINYALA

Ubainisho wa kudhoofika unapendekezwa kama: Kitamkwa x kinasemekana kuwa dhaifu kwa kitamkwa y ikiwa kinapitia mwendo x kikielekea sifuri Ø.

Ili tuweze kujadili suala hili, ingekuwa bora kuanza na uchunguzi wa konsonanti. Katika mkuruba huu, imejadiliwa kwamba konsonanti huweza kupata nguvu au kudhoofika kutegemea mazingira au nafasi

yake katika silabi au maneno. Lakini, kwanza, hebu tuzingatie mabadiliko yatokeayo katika mazingira kativokali katika deta ifuatayo:

sitapu > sitabu > sitaβu > sitawu > sitau "kitabu"
puku > buku > βuku > wuku > uku "buku"

Mifanyiko inayodhihirika hapa ni kativokali mghuno, kativokali kwamiza, kativokali usonoranti na kativokali sonoranti udondoshi. Tumeona:

p > b > β > w > ø

Hata tukiachana na mabadiliko yatokeayo kativokali, tunaweza kupata [b] ikidondoshwa katika deta ifuatayo:

| | |
|---|---|
| [buXakuŋga] > [βuXakuŋga] > [uXakuŋga] | "jina la mahali" |
| [buXana] > [βuXana] > [uXana] | "gita" |
| [buXwe] > [βuXwe] > [uXwe] | "ukwe" |
| [bule] > [βule] > [ule] | "wimbi" |
| [busela] > [βusela] > [usela] | "uji" |
| [bukula] > [βukula] > [ukula] | "chukua" |
| [bula] > [βula] > [ula] | "tambua/twanga" |

Tunachoona hapa ni kwamba:

b > β > ø

[bea] > [βea] "danganya"

[biXa] > [βiXa] "weka"

[bene] > [βene] "wenyewe"

[beXo] > [βeXo] "jamaa"

[bika] > [βika] "tamba"

Tunachoshuhudia ni kuwa [b] hukwamizwa ipatikanapo katika mazingira ya kabla ya vokali za mbele. Kanuni kwa hivyo ni:

$$\begin{bmatrix} +\text{Mtuo} \\ \\ -\text{Kwamiza} \end{bmatrix} \longrightarrow [+\text{Kwamiza}]/__ \begin{bmatrix} +\text{Vokali} \\ \\ -\text{Nyuma} \end{bmatrix}$$


Kitamkwa hupata nguvu ikiwa, tuseme, [p] inayodhoofisha huongezwa nguvu na kuzua [p] mbili yaani [pp]:

$$p \longrightarrow [pp]$$

Kama njia nyingine ya kufafanua kupata nguvu na kudhoofika kwa vitamkwa, tunaweza kupendekeza kwamba vitamkwa vyenye nguvu vina uwezo mkubwa sana wa kupambana na kuhimili michakato ya kudhoofisha. Kwa msingi huu, konsonanti zimeainishwa kulingana na vigezo vya nguvu zake kwa kuzingatia mahali pa kutamkia, jinsi zinavyotamkwa na hali ya glota.

Foley (1977) ametoa kielelezo cha kuainishia unguvu wa vitamkwa. Kielelezo hiki, anasema, ni muhimu katika uchanganuzi wa lugha

za Kijerumani na Kiispania kwa upande wa kubadilishana konsonanti. Kielelezo hicho ni kama ilivyo hapa chini:




Mpangilio wa kwenda kulia unazipanga konsonanti kulingana na mahali pa kutamkia ilhali kwenda juu unazipanga konsonanti kulingana na jinsi zinavyotamkwa na kuwa hafifu au kuwa na mghuno.

Kulingana na Foley, arki za kifonolojia ($k^+$ $t^+$ $p^+$) zinaweza kuainishwa katika hali mbalimbali kifonetiki. Hivyo, zinaweza kuwa kama vituo virefu (kk, tt, pp) au kama sauti za mpumuo ($k^h$, $t^h$, $p^h$) ama vizuio-kwamiza ($k^x$, $t^s$, $p^f$).

Katika mpangilio huu wa Foley, tutaanza kurejelea madai yake kwamba sauti za midomoni zina nguvu kuliko zile za meno na ufizi, ambazo, nazo, zina nguvu kuliko zile za kaakaa laini. Mwanaismu huyu alizingatia sana ushahidi uliopatikana katika Kideni na Kiispania kuonyesha kuwa [b] ina nguvu zaidi ya [d] au [g]. Kutoka Kideni, Foley anasema kwamba sauti za kaakaa laini za

kativokali na zile za meno hudhoofika bali si za midomoni. Alitumia mfano ufuatao kudhihirisha madai yake:

| | | | |
|---|---|---|---|
| | kage | [kaɣe] | "keki" |
| | bide | [biðe] | "uma" |
| lakini | kobe | [kobe] | |

Katika maendeleo ya Kiispania, kulingana na Foley, kativokali [g] na [d] zimedondoka ilhali [b] inabakia ikikwamizwa na kuwa [β] k.m.

| | Kilatini | Kiispania | |
|---|---|---|---|
| | lego | leo | "mimi husoma" |
| | credo | cre'o | "Naamini" |
| lakini | habere | haber | "kuwa na" |

Madai ya Foley yanaonekana kuafikiana na ukweli baada ya kuchunguza mifano kutoka Kideni na Kiispania. Tumeona pia kwamba, katika kudhoofika kativokali, sauti za mtuo hafifu shadda zina nguvu kuliko sauti za mtuo za mghuno, ambazo, kwa upande wake, ni ndefu kuliko vikwamizo vya mghuno, ambavyo vina nguvu kuliko sonoranti za mghuno. Mpangilio wa Foley wa kwenda juu wa aina za konsonanti waonekana kuwa na nia njema. Vile vile, kwa msingi tulio nao, kutokana na mifano kutoka Kideni na Kiispania, mpangilio wa chini kwenda kulia wa mahali pa kutamkia unaonekana kusawiri baadhi ya lugha za ulimwengu.

Walakini, kuna matatizo mawili ambayo yafaa yadokezwe. Kwanza, mpangilio huu unazishughulikia, kwa kiwango fulani, lugha maalum tu bali si mwanda mzima wa lugha za ulimwengu. Kuna ushahidi tosha kuwa sauti za meno zina nguvu kuliko sauti za midomoni na kaakaa laini katika baadhi ya lugha za ulimwengu. Katika Kinyala (K), sauti za kaakaa laini zina nguvu kuliko zile za midomoni, kama vile inavyojitokeza katika deta ifuatayo, tukizingatia maendeleo ya Kinyala (K):

| Kinyala (B) | Kinyala (K) | |
|---|---|---|
| [dede] | [tete] | "panzi" |
| [sipodo] | [sipoto] | "uke" |
| [dala] | [tala] | "mji/boma" |
| [kuda] | [kuta] | "gonga" |
| [geŋa] | [keŋa] | "funga" |
| [βugiri] | [ukiri] | "jina la mahali" |
| [βuɟuaŋa] | [utʃuaŋa] | "jina la mahali" |
| [ɟuma] | [tʃuma] | "wiki" |

Kutokana na deta hiyo, tunaona sauti [d], [g] na [ɟ] zikidhihirisha uwezo wa kustahimili udhoofishaji. Ambapo kitamkwa [d] ambacho ni cha ufizi, [ɟ] ambacho ni cha kaakaa ngumu na [g] ambacho ni cha kaakaa laini, tunaona unguvu wa vitamkwa hivi pale ambapo vinaondolewa mghuno tu na kuwa [t], [tʃ] na [k]. Kitamkwa [b], ambacho ni cha midomoni, kinakwamizwa na hatimaye kupotea kabisa.

Tatizo la pili la Foley linatokana na ukweli kwamba viwango vya kupata nguvu vinatolewa kwa msingi wa mifanyiko ya kudhoofika, ambayo ni ya aina ya kipekee. Swala la mazingira ambayo kudhoofika kunatokea halijashughulukiwa vya kutosha. Tunachojua ni kwamba njia ya kawaida kabisa na ya mwisho katika mfanyiko wa kudhoofika ni kufifia au kuondoa mghuno. Maadam mfanyiko huu unaigeuza [b] na kuwa [p], halafu sifuri ∅, [b] katika mazingira haya yafaa ichukuliwe kama iliyo na nguvu kuliko [p] ingawa katika mazingira ya kativokali tumeiona kuwa inadhoofika.

Kwa mintarafu hii, ni heri tuhitimishe sehemu hii kwa kusema kwamba uchanganuzi kama ule wa Foley ni muhimu, si tu kwa tofauti zilizoko katika lugha maalum lakini, pia, kwa mazingira halisi ambamo vitamkwa hutokea.

### 4.4 USAWAZISHO CHANGAMANO KATIKA KINYALA

Usawazisho changamano ni mfanyiko wa kifonolojia ambao uainisho wa kifonolojia hupunguzwa katika mazingira fulani. Vitamkwa vinavyotofautiana, katika mazingira sawa, vina uwakilisho sawa katika mazingira ya usawazisho changamano.

Dhana ya usawazisho changamano ni muhimu katika uchanganuzi wa fonimu kama kikundi cha sauti, na pia kuzingatia utendakazi wake katika mfumo wa kifonolojia unaokinzana. Hii ni kwa sababu usawazisho changamano hutusaidia kuelezea hali ambapo foni fulani inaweza, wakati fulani, kuhusishwa na fonimu moja na, kwa kiwango kingine, na fonimu nyingine. Mfanyiko huu unajulikana kama usawazisho wa kifonimiki. Katika Kinyala (K), fonimu /l/ na /r/,

katika mazingira ya mwanzo ya silabi hutamkika kama [l] na [r], kama vile ilivyo hapa chini:

| | | |
|---|---|---|
| lia | [lia] | "kula" |
| ria | [ria] | "ogopa" |
| lisia | [lisia] | "lilisha" |
| risia | [risia] | "kemea k.m. mashetani" |

Katika mazingira ya kativokali, /l/ inatamkika kama /r/ kama vile inavyojitokeza katika deta ifuatayo:

| | | | |
|---|---|---|---|
| lela | /lela/ | [lera] | "lea" |
| lila | /lila/ | [lira] | "lia" |
| usela | /usela/ | [usera] | "uji" |
| tekhela | /teXela/ | [teXera] | "pikia" |

Katika hali hii ya usawazisho wa kifonimiki, fonimujumuishi huundwa kuwakilisha vitamkwa hivyo. Fonimujumuishi ni sehemu ya kifonolojia ambayo huchukua sifa zote za kifonolojia zinazohusisha fonimu mbili. Fonimujumuishi ambayo huandikwa kama herufi inajitokeza kama ifuatavyo:

/lela/ ⟶ leLa
/lila/ ⟶ liLa
/usela/ ⟶ useLa
/teXela/ ⟶ teXeLa

## 4.5 TABDILI KATIKA KINYALA

<u>Kamusi Sanifu ya Ismu na Lugha</u> (1990) inapambanua tabdili kama hali ya sauti mbili kubadilishana nafasi katika neno. Hata hivyo, kwa minajili ya kazi yetu, ni muhimu tuongezee kwamba tabdili huweza kuhusisha kubadilishana nafasi ya zaidi ya sauti mbili katika neno. Katika Kinyala (K) sauti mbili zinazobadilishana nafasi zinajitokeza katika:

| | | | |
|---|---|---|---|
| [tajwa] | → | [twaja] | "jogoo" |
| [siβiriti] | → | [siriβiti] | "kiberiti" |
| [tajarisa] | → | [tarajisa] | "tayarisha" |

Katika deta hii, tunaona [β] ikibadilishana nafasi na [r] na [w] ikihamishwa. Matokeo hapa ni kwamba kubadilishana nafasi kwa sauti hizo hakuna athari zozote kisemantiki - maana inabakia ile ile tu. Walakini, tabdili inayohusisha sauti zaidi ya moja husababisha mabadiliko ya kisemantiki katika Kinyala (K) kama vile inavyojitokeza katika deta ifuatayo:

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| [tʃaXo] | "wekelea" | → | [Xotʃa] | "mjomba" |
| [manu] | "halafu" | → | [numa] | "ninauma" |
| [lama] | "laani" | → | [mala] | "maliza" |
| [siosi] | "ni nini" | → | [sisio] | "ni chako" |
| [ŋgese] | "kama mimi" | → | [seŋge] | "shangazi" |
| [Xaka] | "jaribu" | → | [kaXa] | "nuka k.m. mboga" |
| [laβa] | "kuwa safi" | → | [βala] | "hesabu" |
| [kava] | "gawa" | → | [vaka] | "chuna ngozi" |
| [siasa] | "siasa" | → | [sasia] | "tawanya" |
| [lasa] | "tupa" | → | [sala] | "omba/sumbuka" |
| [lamwa] | "laaniwa" | → | [mwala] | "mnatandika" |

## 4.6 USIGANO KATIKA KINYALA

Katika lugha, sauti ambazo hapo awali zilikuwa zinafanana, kwa kiasi fulani, huishia kutofautiana. Jambo hili litokeapo, basi, huo ndio usigano. Katika deta ifuatayo, tunaona usigano katika Kinyala (K):

| | | | |
|---|---|---|---|
| ntsanu | → | njanu | "ni nani" |
| ntseve | → | njeve | "niulize au aina ya kiti" |
| ntsietsi | → | njiechi | "ndizo hizi" |
| ntsia | → | njia | "ninaenda" |
| ntsula | → | njula | "ninatoka" |
| ntsukha | → | njukha | "ninamwaga au nyoka" |
| tsia | → | chia | "enda" |
| tseva | → | cheva | "uliza" |
| tsula | → | chula | "toka" |
| tsukha | → | chukha | "mwaga" |
| yitsa | → | yicha | "njoo/kuja" |
| bitsa | → | bicha | "pita" |
| batsa | → | bacha | "kwepa" |
| kwatsia | → | kwachia | "funga kwa ustadi" |

Tunachoona katika deta hii ni kwamba, katika Kinyala (K), matumizi ya [ts] yalishabihiana na [tʃ] au [ɟ]. Walakini, tofauti hizo hivi sasa zimegubikwa kiasi kwamba tumebakia na [tʃ] na [ɟ] tu. Katika mkuruba huu, kanuni zinazojitokeza ni:

a) ts ——→ ɟ/N___ k.m. ntsanu ___ njanu

ntseve ___ njeve

b) ts $\longrightarrow$ tʃ/#___ k.m. tsukha ____ chukha

tsula ____ chula

c) ts $\longrightarrow$ tʃ/V - V k.m. yitsa ____ yicha

bitsa ____ bicha

Kinachodhihirika ni usigano wa aina tatu: usigano mbele, kama vile katika (a); usigano nyuma, kama vile katika (b); na usigano kativokali, kama vile katika (c).

**4.7 HAPLOLOJIA KATIKA KINYALA**

Kulingana na <u>Kamusi Sanifu ya Ismu na Lugha</u> (1990), haplolojia ni tendo la kuacha kitamkwa kimoja au zaidi endapo kinafanana na kitamkwa kinachofuatia au kinachokitangulia. Katika Kinyala (K) kuna:

a) mwa + ana $\longrightarrow$ mwana "mtoto"

ba + ala $\longrightarrow$ bala "hesabu"

b) mwe + ekesia $\longrightarrow$ mwekesia "mwalimu"

mbe + ese $\longrightarrow$ mbese "nipe mimi"

c) si + imba $\longrightarrow$ simba "kizimba"

si + isala $\longrightarrow$ sisala "kiti"

d) mwo + kho $\longrightarrow$ mwokho "utapia mlo"

mwo + oko $\longrightarrow$ mwoko "mhogo"

e) mu + ulindi $\longrightarrow$ mulindi "mchungaji k.m. kidini"

mu + uya $\longrightarrow$ muya "hewa/pumzi"

Katika deta (a), tunaona udondoshi wa vokali [a] pale ambapo zinafuatana; katika deta (b) tunaona udondoshi wa vokali [e] pale ambapo zinafuatana; katika deta (c) tunaona udondoshi wa vokali [i]; katika deta (d) tunaona udondoshi wa vokali [o]; na katika deta (e) tunashuhudia vokali [u] ikidondoshwa. Kinachojitokeza, kwa hivyo, ni kuwa udondoshi wa kihaplolojia katika Kinyala (K), aghalabu, huhusisha vokali - vokali moja hudondoshwa zinapofuatana mbili zinazofanana.

**4.8 SANDHI KATIKA KINYALA**

<u>Kamusi Sanifu ya Ismu na Lugha</u> (1990) inaeleza sandhi kama badiliko la sauti litokanalo na sauti nyingine jirani; kunywea kwa neno au kudondoshwa kwa baadhi ya sauti katika ufupishaji wa neno hilo. Sandhi inaweza kupambanuliwa na deta ifuatayo katika Kinyala (K):

| | | | |
|---|---|---|---|
| Mberesekho | → | mbekho | "Tafadhali nipe" |
| chichanga | → | chianga | "Uwe ukienda" |
| mbulilire | → | mbulire | "nisikizeni" |

Athari za uradidi wa [tʃ] na "li" unasababisha kudondoshwa mojawapo.

## 4.9 HITIMISHO

Katika sura hii, mifanyiko ya kifonolojia idhihirikayo katika Kinyala (K) imejadiliwa. Imeonyeshwa kwamba mifanyiko ya kifonolojia itokeayo katika Kinyala (K) ni ya aina nane, ambayo ni wiano, mifanyiko ya miundo ya silabi, kudhoofika na kupata nguvu, usawazisho changamano, tabdili, mpinduo, usigano, haplolojia na sandhi. Zaidi ya hayo, mifanyiko hiyo imeelezwa kiisimu kwa kuiundia kanuni zinazoitawala.

# SURA YA TANO

## MAPENDEKEZO NA HITIMISHO

### 5.0 UTANGULIZI

Katika sura hii ya tano, mambo muhimu yaliyoibuka na kubainika kutokana na utafiti huu yataelezwa. Kisha, matatizo na mafanikio yaliyopatikana katika utafiti huu yataelezwa. Halafu, hitimisho litapatikana kwa kutoa mapendekezo kuhusu sehemu zinazohitaji kufanyiwa utafiti zaidi.

### 5.1 KAZI KWA JUMLA

Utafiti huu ulijishughulisha na kuchunguza mifanyiko ya kifonolojia katika Kinyala cha Kakamega. Katika uchunguzi huu, iligunduliwa kuwa Kinyala (K) kina fonimu ishirini na nane - konsonanti ishirini na tatu na vokali tano. Konsonanti hizo ni /b, β, d, f, g, ŋ, h, ɟ, tʃ, k, X, l, m, ɱ, n, ɲ, p, r, s, t, v, w, j/ ilhali vokali ni /a, e, i, o, u/. Utafiti huu ulizieleza sauti hizi kiisimu na mifanyiko itokeayo. Hatimaye, utafiti huu pia ulionyesha jinsi mifanyiko hiyo inavyodhihirika kwa kuiundia kanuni ambazo hufuatwa kufikia mifanyiko hiyo.

Zaidi ya hayo, katika malengo ya jumla, utafiti huu ulitoa jawabu kwa maswali kemkem ambayo yalikuwa kama mwongozo katika utafiti. Kwanza, mifanyiko ya kifonolojia katika Kinyala (K) iligunduliwa. Iligunduliwa kwamba Kinyala (K) hudhihirisha mifanyiko ya kifonolojia. Kwa hivyo, kwa kujibu swali ikiwa lahaja ya Kinyala (K) hudhihirisha mifanyiko ya kifonolojia, utafiti huu ulionyesha

kuwa Kinyala (K) hudhihirisha mifanyiko ya kifonolojia ya aina nane: wiano; miundo ya silabi; kudhoofika na kupata nguvu; tabdili; usigano; haplolojia; na sandhi.

Wiano wa aina nne ulijitokeza ambapo:

a) konsonanti huwiana na sifa za vokali;

b) vokali huwiana na sifa za konsonanti;

c) konsonanti huwiana na sifa za konsonanti; na

d) vokali huwiana na sifa za vokali (tangamano vokali).

Mifanyiko ya miundo ya silabi ilijitokeza kama:

a) kudondoshwa kwa konsonanti;

b) kudondoshwa kwa vokali;

c) uchopekaji wa konsonanti;

d) uchopekaji wa vokali;

e) muungano wa konsonanti; na

f) muungano wa vokali.

Kuhusu kudhoofika na kupata nguvu, iligunduliwa kwamba mifanyiko hii hudhihirika katika Kinyala (K) kama: kativokali mguno; kativokali kwamiza; kativokali usonoranti; na kativokali sonoranti udondoshi.

Usawazisho changamano katika Kinyala (K) huhusisha sauti /l/ na /r/ na kuzua fonimujumuishi L. Tabdili huhusisha sauti mbili kubadilishana nafasi au sauti zaidi ya mbili. Sauti mbili zibadilishanapo nafasi, hakutokei tofauti kimaana. Walakini, sauti zaidi ya mbili zinapobadilishana nafasi kunatokea tofauti

kimaana. Usigano udhihirikao katika Kinyala (K) ni wa aina tatu: usigano mbele; usigano nyuma; na usigano kativokali. Haplolojia, katika lahaja hii, aghalabu, huhusisha vokali ambapo vokali moja hudondoshwa zinapofuatana mbili zinazofanana. Kwa upande wake, sandhi huhusisha kudondoshwa kwa baadhi ya sauti katika ufupishaji wa neno husika.

Pili, utafiti huu ulitarajiwa kuonyesha kwamba, katika lahaja hii, mifanyiko itokeayo ni ya kifonimiki. Ilionekana kuwa mingi ya mifanyiko ya kifonolojia katika lahaja hii ni ya kifonimiki isipokuwa ile iliyo na uhusiano wa karibu na semantiki, kama vile tabdili.

Mwisho, kuhusu jinsi ya kuweza kuisawiri na kuieleza mifanyiko ya kifonolojia katika Kinyala (K) kiisimu na kuonyesha kanuni za kifonolojia ziwezazo kueleza mifanyiko hiyo, Ilionekana kuwa kanuni za kiisimu zimezingatiwa katika kueleza mifanyiko hiyo na pia kuiundia kanuni mahsusi.

## 5.2 MAFANIKIO NA MATATIZO

Mifanyiko ya kifonolojia katika Kinyala (K) imeelezwa ka tafsili. Mifanyiko hiyo pia imeundiwa kanuni za kifonolojia ziwezazo kutumiwa kuelezaa mifanyiko hiyo na, hivyo, kuieleza kiisimu.

Hata hivyo, kulikuwa na utata ambapo wengi wa Wanyala walioshughulikiwa walishindwa kueleza kile kilichosababisha mfanyiko wa usigano ambapo [ts] ilibadilishwa na mahali pake pakachukuliwa na [tʃ] na [ɟ] na [r]. Kuna wale waliodai kwamba

sauti [ts] ilikuwa ikitamkwa kwa sababu Wanyala walipokuwa Busia, walikuwa waking'oa meno. Tatizo hapa ni kwamba je, [tʃ] ni sauti ya meno? Kuna wengine waliodai kwamba Wanyala waliamua kutumia [tʃ] na [dʒ] kwa sababu ndio mtindo wa Waluyia wengine, kama vile Wabukusu na Wanyore, waliohusishwa nao zamani. Walakini, iligunduliwa kwamba, ijapokuwa Wanyala wanakurubiana na Wabukusu, Wanyore ni kundi lililo mbali sana na Bunyala (K). Isitoshe, ukuruba uliopo kati ya Wanyala na Wawanga, Watsotso na Wakabras ni mkubwa kuliko ule walio nao na Wabukusu. Kati ya Wanyala na Wabukusu, kuna kizuizi kikubwa cha kijiografia - Mto Nzoia. Hali hii ni tofauti tunapolinganisha ukuruba wa Wanyala na Wawanga, Watsotso na Wakabras ambao hutumia [ts] bali si [tʃ] au [dʒ]. Kilichojitokeza ni kwamba kulikuwa na tukio la kihistoria katika lugha ambalo linahusiana na kupoteza au kubadilisha sauti.

Hata hivyo, ingawa kulikuwa na matatizo madogomadogo kama hayo, utafiti huu, kwa kiasi kikubwa, umefanikiwa kutupatia majibu ya yale maswali yaliyokuweko mwanzoni mwa utafiti huu.

**5.3 MAPENDEKEZO NA HITIMISHO**

Kutokana na uchunguzi huu, ni muhimu kurejelea sana dhana ya Schane (1972) kuhusu umuhimu wa makundi ya mifanyiko ya kifonolojia. Schane anasisitiza haja ya kuzua na kuendeleza nadharia dhahiri ya makundi haya. Kwa mfano, kuna haja ya uibuaji wa nadharia ya wiano kudhihirisha ni vipandesauti vipi au vya aina gani vinavyowiana na mwelekeo wake (wiano mbele au nyuma). Nadharia ya muundo wa silabi pia yafaa ionyeshe mpangilio kingazi mwafaka wa aina zake na mifanyiko ya urahisishaji wa silabi.

Kuhusu nadharia ya ubainishi wa hali ya juu, kuna uhitaji wa kutoa kundi la vizuizi ambavyo husababisha usawazisho usiowiana na, vile vile, kuelezea hakika mwelekeo wa usawazisho. Maelezo ya aina hii yatasaidia katika kutolea ithibati za ndani kwa ndani za makundi mbalimbali ya kanuni asilia na kutoa mwangaza juu ya nini kifaacho au kisichofaa kuwa kanuni asilia. Kinachosemekana hapa ni kuwa dhana kwamba lugha hupitia mifanyiko ya kifonolojia ni suala lifaalo kuchunguzwa kwa makini sana.

Kwa mintarafu hii, ni wazi kwamba kuna ukubaliano na maoni ya Schane. Hii ni kwa sababu, kwa kutazama mifanyiko iliyofafanuliwa, bado kunazuka hali ya mparakanyiko kuhusu asilia halisi ya mifanyiko hiyo. Zingatia usemi kwamba uyeyushaji ni aina ya muundo wa silabi unaopendelewa zaidi au uchopekaji wa konsonanti katika muktadha huo. Suala jingine linalojitokeza ni, je, haplolojia na sandhi zinatofautianaje na udondoshi? Mpaka u wapi?

Kwa hivyo, ni muhimu kuhitimisha kwamba utafiti juu ya mifanyiko ya kifonolojia haujitoshelezi. Bado kuna mwanya mkubwa unaoitisha uchunguzi zaidi.

## MAREJELEO


Abercrombie, D. (1965). Studies in Phonetics and Linguistics, Oxford University Press, London.

_________ (1967). Elements of Phonetics, Edinburg University Press, Edinburg City

Anderson, S.R (1974). Organisation of Phonology, Academic Press, New York

__________ (1985). Phonology in the Twentieth Century, University of Chicago Press, London.

Anderson, W.L na Stageberg, N.C. 1962. Introductory Readings on Language, Holt, Rinehart na Winston.

Angogo (1983). Unity in Diversity.

Antila, R. (1972). An Introduction to Historical and Comparative Linguistics, Macmillan, New York.

Arnason, K. (1981). A Diachronic Look at the Syllable Language V.18.

Aswani, F.O.B. (1993). "Fonolojia ya Silabi ya Kiswahili Sanifu na ya Kimarama: Uchunguzi Linganishi," Tasnifu ya M.Phil., (Haijachapishwa), Chuo Kikuu cha Moi.

Bakari, M. (1982). The Morphophonology of Kenyan Swahili Dialects, Tasnifu ya Ph.D., Chuo Kikuu cha Nairobi.

Baldi, P.W Werth, R.N. (1978). Readings in Historical Phonology, Pennisylvia State University Press, University press University park.

Batibo, H.M (1980)."Je Fonolojia ya Kiswahili ni ya kibantu?" Makala iliyosomwa katika semina ya Iringa (Haijachapishwa).

_____________ (1981). "Tutazameje Mfungamano King'ong'o-

Konsonanti katika Kiswahili," Makala yanatarajiwa kuchapishwa na Tuki, Dar es Salam).

Benjamin, J.B.V. (1980). "Issues in Vowel Harmony," CONY Linguistic Conference, Amsterdam.

Bloomfield, L. (1976). Language (13th Impression), George Allen and Unwin Ltd, London.

Brosnahan, L.F.K na Malmberg, B. (1970). Phonetrics, Cambridge University Press, Cambridge.

Bynon, T (1977). Historical Linguistics, Oxford University Press, London.

Chomsky, N. na Halle, M. (1968). The Sound Patterns of English, Harper and Row New York.

Clark J. na Yallop, C. (1990). An Introduction to Phonetics and Phonology. Basil Blackwel, Oxford, London

Conie, B. (1981). Linguistic Universals and Language Typology, Blackwell, Oxford, London.

Crowley, T. (1992). An Introduction to Historical Linguistics, Oxford University press.

Crystal, D (1987). The Cambridge Encyclopaedia of Language, Cambridge University Press, Cambridge.

_______ (1990). A Dictionary of Linguistics and Phonetics, Basil Blackwell, London.

De Blois (1975). Bukusu Generative Phonology and Aspects of Bantu Structure, Musee Royal De L'Afriane Central) Tervuren, Belgigue.

Dell, F (1989). Generative Phonology, Cambridge University Press, Paris.

Dodson, C.J. (1967). Language Teaching and the Bilingual

Method, Sir Isaac Pitman and Sons Ltd, London.

Durand, J. (1990). Generative and Non- Linear Phonology, Croom Helm, London.

Fischer-Jogensen, L. (1975). Trends in Phonological Theory, Akademistk Forlag, Copenhagen.

Foley, J. (1977). Foundations of Theoretical Phonology, Cambridge University Press, Cambridge.

Fromkin, V. na Rodman, R. (1983). An Introduction to Language, C.B.S. College Press, New York.

Fry, D.B. (1970). The Physics of Speech, Cambridge University Press, Cambridge.

Furaha, J.H. 1991. "Matumizi ya Lugha Mjini Malindi: Jinsi Mielekeo Inavyoathiri Uteuzi wa Lugha", Tasnifu ya M.A., Chuo Kikuu cha Kenyatta (Haijachapishwa).

Geng, P.A. (1981). Introduction to Principles of Language, Harperand Row, New York.

Gimson, A.C. (1970). An Introduction to the Pronunciation of English, Edward Arnold, London.

Goldsmith, J.A. (1984). Mauseens Rule: Language Sound Structure, Arnoff and Oehirle (wahariri), MIT Press. Massachusetts.

Greenberg, J. (1963). Universals of Language, MIT Press, Cambridge, Massachusetts.

Guthrie, M. (1967). The Classification of Bantu Languages, Dawson of Pau Mau, London.

_______ (1967). Comparative Bantu. Vol. 1, Gregg, London.

Halliday, M.A. (1964). Linguistic Science and Language, Longman, London.

__________ (1985). An Introduction to Functional Grammar, Edward Arnold, London.

Heine, B. (1976). A Typology of African Languages, Deitrich Reimer Verlag - Berlin.

Herriot, P. (1983). An Introduction to Phonology of Language, Billing and Sons, London.

Hjelmslev. (1970). Language: An Introduction, University of Wisconsin Press, London.

Hock, H.H. (1986). Principles of Historical Linguistics, Monton De Guyter, Berlin.

Hockett, C.F. (1958). A Course in Modern Linguistics, The MacMillan Company, New York.

Hockett, C.G. (1976). An Introduction to Natural Generative Phonology, Academic Press, New York.

Hooper, F.B. (1976). An Introduction to Natural Generative Grammar, Academic Press, New York.

Hyman, L.M. (1975). Phonology: Theory and Analysis, Holt Rhinehart, Winston San Francisco.

Jakobson, R. na Halle, M. (1959). Fundamentals of Language, Monten Press, Hague.

James, C. 1980). Contrastive Analysis, Longman, Singapore.

Jones, W.E. na Laver, J. (wahariri). (1972). Phonetics in Linguistics:ABook of Readings, Longman, London.

Kachru, B.B. na Wengine (wahariri). (1973). Issues in Linguistics, University of Illinois Press.

Kasaya, Z.S. (1992). "Logooli, Wanga and Lubukusu Dialects of Luyia: A Study of the Major Phonological Processes," Tasnifu ya M.A. (Haijachapishwa), Chuo Kikuu cha Nairobi.

Keller, A.R. (mhariri). (1972). A Reader in Historical Linguistics, Holt, Rhinehart & Winston, New York.

Kenstowicz, M. na Kisseberth, C. (1977). Topics in Phonological Theory, Academic Press, New York.

Kess, J.F. (1976). Psycholinguistics: Introductory Perspectives, Academic Press, New York.

King, R.D. (1969). Historical Linguistics and Comparative Grammar, Prentice-Hall, Englewood Cliffs, New Jersey.

Khamis, A.M. (1978). "Matamshi na Maandishi ya Kiswahili," MS. (Haijachapishwa).

Knowles, G. (1987). Patterns of Spoken English: An Introduction to English Phonetics, Longman Inc., New York.

Kreidler. (1987). The Pronunciation of English, Basil Blackwell, London.

Ladefoged, P. (1982). A Course in Phonetics, Harcourt Brace Jovanovich, New York.

Lass, R. (1976). English Phonology and Phonological Theory, Cambridge university Press, London.

______. (1984). Phonology: An Introduction to Basic Concepts, Cambridge University Press, London.

Laver, J. (1972). Production of Speech, Penguin, London

Leontier, A.A. (1981). Psychology and the Language Learning Process, Fergaman Press, Oxford.

Lyons, J. (1981). New Horizons in Linguistics, Penguin, London.

Maganga, C. (1970). "Jinsi ya Kufundisha Matamshi ya Kiswahili kwa Wageni," Makala, Zanzibar.

______ 1982). "Mofofonolojia ya Kiswahili Sanifu, Kipemba,

Kitumbatu na Kimakunduchi," Tasnifu ya Ph.D, (Haijachapishwa", Dar es Salaam.

Martinet, O. (1960). Elements of General Linguistics, Gaber and Faber, London.

Mbaabu, I. (1987). Kiswahili Lugha ya Taifa, Kenya Literature Bureau, Nairobi.

Mwansoko, H.J.M. (1990). "Shadda katika Kiswahili," Makala katika Jarida la Kiswahili JK Na 1, ESC Ltd, Dar es Salaam.

Nchimbi, A.S. (1991). "Je, Mang'ong'o ni Fonimu au si Fonimu katika Kiswahili Sanifu," Makala katika Baragumu, Jarida la Idara ya Kiswahili ya Chuo Kikuu cha Maseno, Kisumu.

___________. (1979). "Le Consonanisme du Kiswahili: Etudes Experimentales Films Radiologigues," Tasnifu ya Ph.D (Haijachapishwa), Chuo Kikuu cha Strasbourg, France.

___________. (1992). "Mfumo wa Matamshi ya Fonimu za Kiswahili," Makala katika Baragumu, Jarida la Idara ya Kiswahili ya Chuo Kikuu cha Maseno, Juzuu 1.

Ngala, J.A. (1992). "A Contrastive Analysis of Dholuo and English Syllable: A Linguistic Approach," Tasnifu ya M.Phil. (Haijachapishwa), Chuo Kikuu cha Moi, Eldoret.

Nyambura, A. (1990)."A Phonology of the Gikuyu Syllable," Tasnifu ya M.A. (Haijachapishwa), Chuo Kikuu cha Kenyatta.

O'connor, J.D. (1973). Phonetics, Hazel and Wartson, Aysbury Bucks.

Palermo, D. (1978). The Psychology of Language, Glenview, Scott and Foreman.

Palmer, L.R. (1972). Descriptive and Comparative Linguistics: A Critical Introduction, Farber and Farber, London.

Pei, M. 1965. Invitation to Linguistics, Henry Regnery Company.

Pike, K.L. (1947). Phonemics: A Techinique for Reducing Languages to Writing, University of Michigan Press, Oklahoma.

Polome, E. (1967). A Handbook of Kiswahili Language, Institute of african and Oriental Studies, London.

Postal, P. (1968). Aspects of Phonological Theory, Harper and Row, New York.

Pratt, M. L. na Tangot, E.C. (1980). Linguistics for Students of Literature, Harcourt Brace Jovanovich Inc., New York.

Roach, P. (1983). English Phonetics and Phonology: A Practical Course, Cambridge University Press, New York.

Robins, R.H. 1967. A Short History of Linguistics, Longman, London na New York.

Schane, S.A. (1972). Generative Phonology, Englewood Cliffs, N.J. Prentice-Hall.

__________. (1972). "Natural Rules in Phonology" katika Stockwell L.R.P. na MaCawley, R. (wahariri) Linguistic Changes and Generative Theory.

Sloat, C. (1978). Introduction to Phonology, Englewood Cliffs, Prentice-Hall.

Smith, N.V. (1973). The Acquisition of Phonology: A Case Study, Cambridge University Press, Cambridge.

Sommerstein, A.N. (1977). Modern Phonology, Edward Arnold, London.

Southworth, F.C. na Daswani , C. J. (1974). Foundations of Linguistics, The Free Press.

Stampe, D. (1979). The Study of Natural Phonology: Current Approaches to Phonological Theory, University of Chicago Press.

Tucker na Ashton. (1942). Swahili Phonetics.

TUKI. (1981). Kamusi ya Kiswahili Sanifu, Oxford University Press, Nairobi.

_______ (1990). Kamusi Sanifu ya Ismu na Lugha, TUKI, Dar es Salaam.

Welmers, E.M. (1973). African Language Structures, University of California Press, London.

Were, G.S. (1967). A History of the Abaluhya of Western Kenya C.1500-1930, East African Publishing House, Uniafric, Nairobi.

Whiteley, W.H. (mhariri). (1974). Language in Kenya, Oxford University Press, Nairobi.

Wilkins, D.A. (1972). Linguistics in Language Teaching, Edward Arnold, London.

Wise, C.M. (1957). Applied Phonetics, Prentice-Hall Inc., London.

## VIAMBATANISHO

### KIAMBATANISHO 1: ALAMA RASMI ZA KIFONOLOJIA

Wakirasmisha kanuni za kifonolojia, wanaismu wamependekeza matumizi ya alama zifuatazo:

a) / humaanisha katika mazingira ya

b) $\rightarrow$ humaanisha inakuwa

c) ___ humaanisha kabla au baada ya kitamkwa

Alama kadhaa za kiismu hutumiwa kurasmisha kanuni za kifonolojia. Baadhi yazo ni:

**Mabano Mraba**

$$\begin{bmatrix} A \\ E \end{bmatrix} \longrightarrow B/___ \begin{bmatrix} C \\ D \end{bmatrix}$$

Mabano haya yanaonyesha kuwa:

A inakuwa B katika mazingira kabla ya C

E inakuwa B katika mazingira kabla ya D

$A \longrightarrow B/___\ C$

$E \longrightarrow B/___\ D$

Yafaa itiliwe maanani kwamba mabano mraba huhitaji kwamba vitamkwa viunganishwe au vihusishwe vile vinavyolingana katika

mabano kwa laini moja. Kinachoweza kupatikana kaida za kifonolojia, sana sana, ni matumizi ya sifa solo hata kama mabano mraba yametumiwa. Hivi ndivyo ilivyo katika mfano ufuatao:

$$\begin{bmatrix} + \text{Vokali} \\ \\ - \text{Konsonanti} \end{bmatrix} \longrightarrow [+ \text{Nasali}]/[+ \text{Nasali}]___$$

**Mabano Upinde**

Mabano upinde hutumiwa katika hali mbili. Kwanza, tunapotaka kujumlisha kanuni na, pili, tunapotaka kuonyesha kwamba kuweko kwa kitamkwa fulani au kimoja si jambo la lazima. Mfano hapa waweza kuwa:

$$A \longrightarrow B/___\ (C)D$$

Kanuni hii yaweza kumaanisha:

$$A \longrightarrow B/___\ CD$$

$$A \longrightarrow B/___\ D$$

Yaani kitamkwa C si cha lazima.

**Mabano Mbinuko**

Mabano mbinuko, kawaida, hutumiwa katika kufupisha kanuni kadhaa. Kwa mfano, kanuni zifuatazo zinaweza kufupishwa kwa kutumia mabano mbinuko:

$$A \longrightarrow B / ___ \; C$$

$$A \longrightarrow B / ___ \; D$$

$$E \longrightarrow B / ___ \; C$$

$$E \longrightarrow B / ___ \; D$$

$$\begin{Bmatrix} A \\ \\ E \end{Bmatrix} \longrightarrow B / ___ \; \begin{Bmatrix} C \\ \\ D \end{Bmatrix}$$

Hii ni njia ya kiitkisadi kuliko mabano ya kawaida.

**Alfa**

Alfa hutumiwa kwa sababu ya itkisadi katika sifa zinazohitajika kuelezea mchakato wa kifonolojia. Tukichukulia, kwa mfano, lugha yenye orodha ya kifonolojia ya vokali /i, e, u, o/, uziada unaojitokeza, ambao unatumika kwa vokali hizi, ni kuwa irabu zisizo za chini zinakubaliana katika kuviringisha na unyuma. Kinachosemwa hapa ni kuwa vokali /i/ na /e/ ni [- nyuma - mviringo] ilhali vokali /u/ na /o/ ni [+ nyuma + mviringo]. Kama hatungekuwa na mfumo halisi wa kuwasilisha ujumbe huu, ingetubidi tueleze kuweko kwa vikwazo viwili vya kitamkwa, ambavyo ni:

a) Ikiwa vokali a ni $\begin{bmatrix} -\ \text{chini} \\ -\ \text{nyuma} \\ V \end{bmatrix}$

$$\downarrow$$

halafu [- mviringo]

b) Ikiwa

$$\begin{bmatrix} -\text{chini} \\ +\text{nyuma} \end{bmatrix}_{V}$$

$$\downarrow$$

halafu $[+\text{mviringo}]$

Kinachoonekana wazi hapa ni kwamba tuanahitaji sifa nane ili kuvieleza vikwazo viwili hivi. Walakini, vikwazo hivi vinahusiana sana na, hivyo basi, yafaa vielezwe kama kikwazo kimoja. Alfa hurahisisha jambo hili kama vile inavyoonekana hapa chini:

Ikiwa

$$\begin{bmatrix} -\text{chini} \\ \alpha\text{nyuma} \end{bmatrix}_{V}$$

$$\downarrow$$

halafu $[\alpha\text{mviringo}]$

Alfa, katika mfano huu, yaonyesha kuwa vitamkwa vyote vyaweza kuwa + au -. Matokeo yote ya alfa yana kima sawa. Ni heri izingatiwe kwamba matumizi ya alfa yametuwezesha kuainisha sifa nne tu.

## KIAMBATANISHO 2: DETA

| | | | |
|---|---|---|---|
| para | "fikiri" | mbara | "ninafikiri" |
| tola | "okota" | ndola | "ninaokota" |
| kana | "tamba" | ngana | "ninatamba" |
| chola | "dondoa" | njola | "ninadondoa" |
| nuna | "nyonya" | | |
| kona | "lala" | ngona | "ninalala" |
| chekha | "cheka" | njekha | "ninacheka" |
| chula | "toka" | njula | "ninatoka" |
| nyama | "nyama' | | |
| nyala | "weza" | | |
| nywa | "kunywa" | | |
| yola | "zoa/fika" | njola | "ninazoa" |
| yenya | "taka" | | |
| yova | "changamka au kuwa chonjo" | | |
| kania | "kataza" | ngania | "ninakataza" |
| kama | "tia tembo maji" | ngama | "ninatia tembo maji" |
| kukhu | "nyanya" | | |
| nga | "kama" | | |
| ng'asa | "enea" | | |
| ng'ala | "kususdia" | | |
| ng'ombe | "ng'ombe" | | |
| hera | "pumua" | | |
| heya | "fanya uasherati" | | |
| mali | "nyeusi" | | |
| nulu | "tamu" | | |
| lulu | "kali k.m. tunda" | | |

| | |
|---|---|
| papa | "baba" |
| siuma | "ushanga" |
| siula | "ngo'a/ruhusu" |
| siema | "kinasimama" |
| sioki | "kali k.m. panga" |
| siaka | "kinapalilia" |
| mwana | "mtoto" |
| mwera | "mabaki ya nafaka ' |
| mwibi | "mwizi" |
| lwala | "ugua/kidole" |
| ndwala | "ninaugua" |
| lweyo | "ufagio" |
| lwana | "pambana au utoto" |
| swekha | "toroka" |
| mwikho | "jamaa/mwiko" |
| kiene | "wenyewe (hali ya ukubwa)" |
| kikie | "yake (hali ya ukubwa)" |
| chiene | "zenyewe' |

kulu "mbingu"

kuku "ufuo"

| | |
|---|---|
| chunju | "vitu (hali ya udogo)" |
| nyuma | "nyuma" |
| nyuni | "ndege/nyuni" |
| ng'ina | "mamake au ninametameta" |
| ng'oni | "mwendo wa pole' |

nuni "ufuta"

(lu)pau "ubao" mbau "mbao"

kova "sindikiza" ngova "ninasindikiza"

kiva "gonga" ngiva "ninagonga"

kuma "jikaze/jikakamue" nguma "ninajikaza/ninajikakamua"

kava "gawa" ngava "ninagawa"

kula "nunua" ngula "ninanunua"

tala "weka dhamana" ndala "ninaweka dhamana"

tula "laumu" ndula "ninalaumu"

tira "shika" ndira "ninashika"

tamba "kuwa fukara" ndamba "nimekuwa fukara"

tima "kimbia" ndima "ninakmbia"

tukha "tusi" ndukha "ninatusi"

tema "jaribu" ndema "ninajaribu"

chala "toa damu kwa ng'ombe" njala "ninatoa damu kwa ng'ombe"

chuka "tawala/kuwa majimaji" njuka "ninatawa/ni majimaji"

chukha "mwaga" njukha "ninamwaga"

lecha "leta" ndecha "ninaleta"

lela "lea" ndela "ninalea"

lusa "tapika" ndusa "ninatapika"

leka "dharau" ndeka "ninadharau"

lekha "wacha" ndekha "ninawacha"

lwika "pembe (umoja) njika "pembe (wingi)"

yuka "tembea kwa kasi" njuka "ninatembea kwa kasi"

yula "chukua upesi" njula "ninachukua upesi"

yava "chimba" njava "ninachimba

ngila "njia"

nguyu "ni huyu"

ngaye "nikataze"

nganya "ninakubali"

ngofu "kuukuu"

ngutu "fupi"

ngokho "kuku'

ngiri "ngiri"

nguke "nyani"

ng'ng'a "dinda"

ng'etwa "ugonjwa wa ziwa la ng'ombe"

ng'eng'a "ramba'

mbuka "ninamaka"

pukha "chafuka" mbukha "ninachafuka"

mbe "nipe"

ndeche "nilete"

khese "nisalimu"

mbere mpe kwa niaba yangu"

ndechere "niletee kw niaba yangu"

khesere "msalimu kwa niaba yangu"

mbese "nipe mimi"

mbona "ninaona"

mona "ninaona"

mbuma "sina"

muma "sina/tembe/mbegu"

chula eyo "toka huko"

chulayo "toka huko"

khesa eyo "salimia huko"

khesayo "salimia huko"

khasira eyo "katalia huko"

khasirayo "katalia huko"

bana "watoto"

Bafurika "Wafrika"

lianga "uwe ukila"

lichanga "uwe ukila"

chianga "uwe ukienda"

chichanga "uwe ukienda"

Mwafrika Mwafurika

maalum maalumu

labda laputa

rocket roketi

socket soketi

bag paka

ng'ang'a "dinda"

khong'a "gonga"

meno "meno"

moni "macho"

mangi "mengi"

sitabu sitau "kitabu"

buku uku "buku"

Bukhakunga Ukhakunga "jina la mahali"

bukhana ukhana "gita"

bukhwe ukhwe "ukwe"

bule ule "wimbi

busela usela "uji"

bukula ukula "chukua"

bula ula "tambua/twanga"

boe oe "fungeni"

bona ona "ona"

bola ola "oza"

bosia osia "tongoza"

| | | |
|---|---|---|
| bonga | onga "chelewa kabisa" | |
| becha | "marafiki" | |
| bea | "danganya" | |
| bikha | "weka" | |
| bene | "wenyewe" | |
| bekho | "jamaa" | |
| bika | "tamba" | |
| dede | tete | "panzi" |
| sipodo | sipoto | "uke" |
| dala | tala "mji/boma" | |
| kuda | kuta "gonga" | |
| geng'a | keng'a | "funga" |
| Bugiri | Ukiri | "jina la mahali" |
| Bujwang'a | Uchwang'a | "jina la mahali" |
| juma | chuma | "juma" |
| lia | "kula" | |
| ria | "ogopa" | |
| lisia | "lilisha" | |
| risia | "kemea k.m. mashetani" | |
| lela | lera "lea" | |
| lila | lira "lia" | |
| usela | usera | "uji" |
| tekhela | tekhera | "pikia" |
| taywa | twaya | "jogoo" |
| sibiriti | siribiti | "kibiriti" |
| tayarisa | tarayisa | "tayarisha" |
| chakho | "wekelea" | |
| khocha | "mjomba" | |

| | | |
|---|---|---|
| manu | "halafu" | |
| numa | "ninauma" | |
| lama | "laani" | |
| mala | "maliza" | |
| siosi | "ni nini" | |
| sisio | "ni chako" | |
| ngese | "kama mimi" | |
| senge | "shangazi" | |
| khaka | "jaribu" | |
| kakha | "nuka k.m. mboga" | |
| laba | "kuwa safi" | |
| bala | "hesabu | |
| kava | "gawa" | |
| vaka | "chuna ngozi" | |
| siasa | "siasa" | |
| sasia | "tawanya" | |
| lasa | "tupa" | |
| | | |
| sala | "omba/sumbuka" | |
| lamwa | "laaniwa" | |
| mwala | "mnatandika" | |
| ntsanu | njanu | "ni nani" |
| ntseve | njeve | "niulize |
| ntsietsi | njiechi | "ndizo hizi" |
| ntsia | njia "ninaenda" | |
| ntsula | njula | "ninatoka" |
| ntsukha | njukha | "ninamwaga" |
| tsia | chia "enda" | |

| | | |
|---|---|---|
| tseva | cheva | "uliza" |
| tsula | chula | "toka" |
| tsukha | chukha | "mwaga" |
| yitsa | yicha | "njoo/kuja" |
| bitsa | bicha | "pita" |
| batsa | bacha | "kwepa" |
| kwatsia | kwachia | "funga kwa ustadi" |

mwana mtoto

mwayi "mchungaji

mwekesia "mwalimu"

mwesi "mwezi/nyote"

mwibi "mwizi"

mwichi "muuaji"

mwoko "mhogo

mwokho "utapia mlo"

mulindi "mchungaji k.m. kidini"

muya "hewa/pumzi"

bala "hesabu

simba "kizimba"

sisala "kiti"

| | | |
|---|---|---|
| mberesekho | mbekho | "tafadhali nipe" |
| chichanga | chianga | "uwe ukienda" |
| mbulilire | mbulire | "nisikizeni" |

KIAMBATANISHO 3: BAJETI

**A) Mahitaji ya Kuandika**

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. Makaratasi ya kuandika mafungu 4 @ Sh. 250 | = | Ksh. | 1000.00 |
| 2. Makaratasi ya uchapishaji " " @ Sh. 350 | = | Ksh. | 1400.00 |
| 3. Makaratasi ya kutolesha makala ""@ Sh. 400 | = | Ksh. | 1600.00 |
| 4. Kinasasauti 1 | = | Ksh. | 8000.00 |
| 5. Kanda za kunasia sauti 20 @ Sh. 120 | = | Ksh. | 2400.00 |
| 6. Mawe ya redio 24 @ Sh. 35 | = | Ksh. | 840.00 |
| 7. Vyombo vya kuandikia (kalamu, penseli n.k) | = | Ksh. | 300.00 |
| **JUMLA** | **=** | **Ksh.** | **15,540.00** |

**B) Utafiti Mwandani**

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. Uchunguzi awali | = | Ksh. | 4000.00 |
| 2. Watafiti waandamizi wawili @ Sh. 2000 | = | Ksh. | 4000.00 |
| 3. Ukusanyaji deta | = | Ksh. | 4000.00 |
| **JUMLA** | **=** | **Ksh.** | **12,000.00** |

**C) Usafiri**

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. Ziara tatu Nairobi @ Sh. 400 | = | Ksh. | 1200.00 |
| 2. Siku 15 Nairobi @ Sh. 70 | = | Ksh. | 1050.00 |
| 3. Ziara moja Chuo Kikuu cha Moi | = | Ksh. | 500.00 |
| 4. Ziara mbili Malaha @ Sh. 1000 | = | Ksh. | 2000.00 |
| 5. Ziara mbili Navakholo @ Sh. 800 | = | Ksh. | 1600.00 |
| 6. Siku 15 Malaha @ Sh. 70 | = | Ksh. | 1050.00 |
| 7. Siku 50 Navakholo @ Sh. 70 | = | Ksh. | 3500.00 |
| **JUMLA** | **=** | **Ksh.** | **10,900.00** |

**D) MALAZI NA CHAKULA**

| | |
|---|---|
| 1. Siku 15 Nairobi @ Sh. 500 | = Ksh. 7500.00 |
| 2. Siku 15 Malaha @ Sh. 500 | = Ksh. 7500.00 |
| 3. Siku 50 Navakholo @ Sh. 300 | = Ksh. 15000.00 |
| 4. Siku 5 Eldoret @ Sh. 500 | = Ksh. 2500.00 |
| **JUMLA** | **= Ksh. 32,500.00** |

**E) UCHANGANUZI WA DETA**

| | |
|---|---|
| 1. Malipo ya kazi | = Ksh. 2000.00 |
| 2. Kazi ya komputa | = ksh. 5000.00 |
| **JUMLA** | **= Ksh. 7,000.00** |

**F) UANDISHI WA TASNIFU**

| | |
|---|---|
| 1. Upigaji taipu kurasa 150 @ Sh. 30 | = Ksh. 4500.00 |
| 2. Utoleshaji makala (7) @ Sh. 4 | = Ksh. 5200.00 |
| 3. Kuunganisha katika jarida (7) @ Sh. 300 | = Ksh. 2100.00 |
| **JUMLA** | **= Ksh. 11,800.00** |

**G) Matumizi ya hapa na pale = Ksh. 1,500.00**

**MAKISIO YOTE KWA JUMLA = KSH. 90,740.00**

## KIAMBATANISHO 4: RATIBA YA UTAFITI

1. AGOSTI 1994

   Uwasilishaji wa pendekezo katika Idara na Kitivo

2. SEPTEMBA - OKTOBA 1994

   a) Uchunguzi awali

   b) Yaliyoandikwa juu ya somo hili

   c) Kuajiri na kuwapa mafunzo watafiti waandamizi

3. NOVEMBA - DESEMBA 1994

   Utafiti mwandani

4. JANUARI 1995

   Uchanganuzi wa deta

5. FEBRUARI - MACHI 1995

   Uandishi wa tasnifu

6. APRILI 1995

   Marekebisho na wasimamizi

7. MEI 1995

   Kuwasilishwa kwa tasnifu